

NYOTA



Kevin Akong'o Shikuvale

Kimechapishwa na:



Williams Publishers Limited

Barua Pepe: *williamspublishersltd@gmail.com*

© Kevin Akong'o Shikuvale

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna ruhusa ya kutoa sehemu ya nakala hii au nakala nzima bila ya idhini mahsusi kutoka kwa waandishi.

Kimechapishwa mara ya kwanza 2024

ISBN: 9789966955388

DIBAJI

Kama ilivyo nyota angani, hung'aa bila shuruti na hata usipotaka kuiona utaiona. Vivyo hivyo, Tamthilia ya NYOTA inamulika jamii kupitia yaliyomo ndani yake kwa nia ya kuikomboa jamii kupitia viongozi waadilifu na wenye maono kwa jumuiya nzima. Hawa ni viongozi waliobaidika kwa kila hali na namna anavyotawala MTEMI. Wameuambaa ubinafsi na unajisi mwingine ule unaoendelezwa na Mtemi. Hata hivyo, kuna baadhi ya viongozi kama MTEMI katika nchi za Bara Afrika ambao bado wanajiimarisha mashinani na hivyo basi kuzidi kupanda na kuzalisha matawi ya ukandamizaji na unyanyasaji wa raia wake bila kujali.

Kwa kithibitisha hili, Tamthilia ya NYOTA iliyosanwa na mtunzi KEVIN AKONG'O inamulika kwa uwazi maswala ya ukandamizaji na unyanyasaji yanayofanyiwa raia wa nchi ya SARINA chini ya utawala wa kiimla wake MTEMI.

Kabla ya ujio wa Wakoloni barani Afrika, Waafrika wenyewe walikuwa na mifumo yao ya kiutawala ambayo baadhi yake ilikuwa ya unyanyasaji wa wanajamii. Hivyo basi ujio huu wa Wakoloni ulizidi kuimarisha unyanyasaji

na ukandamizaji wa Waafrika na hatimaye kuongeza idadi ya viongozi wa aina hii hasa wale walioshirikiana na Wakoloni (vibaraka) katika utawala wao.

Kwa ufafanuzi huu mfupi, ni dhahiri kwamba Wakoloni wakongwe waliacha vidonda sugu na makovu mioyoni mwa Waafrika ambao walipambana dhidi ya utawala wa kikoloni. Katika harakati hizi za kujikomboa, wapo wale walioambulia kufungwa jela kama vile NELSON MANDELA na JOMO KENYATTA. Katika tamthilia hii ya NYOTA, Noelah, Mama Noelah na Baba Dora nao pia walifungwa jela kutokana na juhudi zao za kupambania haki. Kuna wale waliouliwa kama vile Baba Noelah na Sarah. Vizalia wa ukoloni mkongwe katika tamthilia hii ni Mtemi na Choche.

Katika mapambano yoyote yale yanayohusisha upinzani lazima watu wapoteze maisha kama ilivyokuwa kwa baadhi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sarina.

Mtunzi wa tamthilia hii hajaishia kwa kueleza matatizo yanayojitokeza kutokana na uongozi mbaya tu bali pia ameonyesha suluhu yake kwa kuwaibua wanaharakati

wa mapinduzi kama vile: Noelah, Sarah, Tito, Toba na Wanafunzi wa Chuo Kikuu.

Harakati hizi zilizaa matunda pale ambapo watumishi wa Ofisi kuu ya Muungano wa Mataifa wanamfikisha MTEMI mahakamani ili kujibu tuhuma za uovu aliofanyia raia na uongozi wake unafika mwisho. Hili ni funzo kwa raia kwamba iwapo viongozi wa aina hii watazidi kukumbatiwa katika nchi zetu bila kuwapiga vita basi tutarajie kuwa na viongozi wajao wenye hulka za kikasuku kama MTEMI na CHOCHÉ.

Kongole za dhati kwa Mtunzi Kevin Akong'o kwa kuonesha waziwazi namna ya kung'oa mamlakani viongozi dhalimu kama MTEMI. Aidha, mtunzi ameinogesha kazi hii kwa kutumia ubunifu wa utomelezi kutokana na matumizi ya USHAIRI ndani ya kazi ya tamthilia hii. Hiki ni kipaji adimu na weledi murua kuwahi kutokea kwenye baadhi ya kazi za tamthilia za Kiswahili. Imekithiri fani na maudhui adimu katika ulingo wa fasihi ambayo yanawafaa sana walimu, wanafunzi na wapenzi wa Fasihi na Lugha ya Kiswahili kwa jumla.

Kevin Akong'o ametuonyesha kuwa ushirikiano ndio nyenzo ya kutokomeza Uongozi mbaya katika nchi zetu barani Afrika. Na iwapo tutakosa umoja na ushirikiano basi tutabaki kujutia na kujisemea: "Ilikuwa bora kabla ya Uhuru kwa sababu tulitarajia makubwa mema lakini sasa hatuna cha kutarajia."

Imeandaliwa Na:

Happy Mademla

Mwalimu na Mwanafasihi

Simu Na: +255719622714

TANZANIA.

Na kuhaririwa

Na: Naluchesi Nyongesa

Mwalimu wa Fasihi na Kiswahili

Simu Na: 0725904197

KENYA

WAHUSIKA

Ndwea: Mtemi, kiongozi wa nchi.

Choche: Naibu mtemi.

Toba: Mkuu wa sheria.

Noelah: Mwanamapinduzi.

Dorah: Rafikiye Noelah.

Sarah: Mwanafunzi wa Chuo Kikuu.

Tito: Mwanafunzi wa chuo kikuu.

Tembo: Mwanawe Choche.

Mganga

Mfungwa 1

Mfungwa 2

Askari 1

Askari 2

Askari mzungu

Mzungu 1

Mzungu 2

Sauti

Mahali: Taifa dhahania la kiafrika - Sarina

Wakati: Takriban miongo sita baada ya uhuru kwa nchi za Afrika.

SEHEMU YA 1

ONYESHO LA KWANZA

(Ni saa moja asubuhi. Paa la nyumba ya marehemu mzee Mkosi linaonekana, limeliwa na kutu kiasi. Nyuta kwenye kuta za nyumba zinaonyesha mianya kadhaa iliyojipasukia. Kuna maua kando kando ya nyumba ambayo yana kila dalili ya kuzeeka. Baadhi ya majani ya maua yale yameangukia kaburi lililoko mbele ya nyumba upande wa kushoto. Ndani mnapomlikwa, meza mbili na viti vitano vinaonekana. Vibuyu vitatu vya maji vinaonekana kwenye kipembe cha nyumba upande wa kushoto. Kile kisicho na maji kimejilalia katikati ya miguu minne ya meza. Meza hii imezungukwa na viti viwili halafu meza nyingine imezungukwa na viti vingine vitatu. Noelah ameketi kwenye kiti mojawapo ya vile vitatu huku katia mkono shavuni. Anainuka na kuanza kutembea tembea ndani ya sebule bila mwelekeo kamili. Anaketi juu ya meza iliyo na kibuyu chini yake na kisha anainamisha kichwa. Mara anaufunika uso wake kwa viganja vya mikono na kisha anainamisha kichwa zaidi hadi mapajani. Anasimama ghafla kwa kushtuka. Anaanza kuvisogeza viti bila mpangilio. Mbisho unasikika mlangoni. Anaingia Dorah.)

Dorah: Sabalkheri Noelah?

Noelah: Akheri. *(Wanakumbatiana)*

Dorah: *(Akimwachilia)* Vipi wewe dada?

Noelah: Nini?

Dorah: Mbona u mnyonge kiasi hiki? Ni maradhi gani yanakusumbua?

Noelah: Mengi tu. *(Akimsogezea kiti)* Keti. *(Dorah anaendelea kumtazama)* Vipi? Naomba uketi. Karibu nyumbani.

Dorah: *(Huku akiketi)* Haya basi niambie ni ndwele zipi hizi. Malaria au pepo punda?

Noelah: Si malaria wala pepo punda.

Dorah: Ni nini basi?

Noelah: Wala siugui pekee. Tunaugua sote.

Dorah: Una maana gani?

Noelah: Kwamba maradhi yamekita mizizi.

Dorah: Sikuelewi.

Noelah: Nimesema si malaria wala pepo punda, si virusi vya ukimwi wala virusi vya korona.

Dorah: Ndio kumaanisha hayajulikani maradhi yenyewe?

Noelah: *(Akisimama)* Yasikupe shaka. *(Anaondoka sebuleni. Dorah anajaribu kuangaliampangilio wa nyumba. Anaonekana kutoridhika. Mara anapoyarudisha macho mezani anakutana*

na picha ya mamake Noelah. Noelah anarudi huku amebeba vikombe viwili vya chai. Anavitia mezani.) Karibu chai.

Dorah: *(Huku bado ameishika picha) Asante. (Huku akipiga fundu) Lakini dada?*

Noelah: Vipi?

Dorah: Naona mambo hapa si ya kawaida.

Noelah: Si wayajua? Wataka pia nikueleze? Au wewe si mwenye macho asiyeambiwa tazama?

Dorah: Noelah kukicha kumekucha, kubali mambo jinsi yalivyo kisha uendeleo kulisukuma gurudumu la maisha. Hujui kwamba maisha ni mkufu? Kuzidi kujipa sonono ni kuyaita mauko yalipo.

Noelah: *(Akiinuka) Dorah, pamepasuka na sioni nikipashona. (Anafungua mlango na kuashiria kuliko kaburi la babake) Tazama. Isitoshe sasa hivi mamangu ni mfungwa. Nifanyeje mimi binti Mkosi?*

Dorah: Yuko jela mamako? Wamemsingizia nini?

Noelah: Ndio, niliona vijikaratasi vya picha iliyoonyesha mke akimuua mmewe. Picha zenyewe zimehaririwa.

Dorah: *(Kwa mshangao) Mambo ya babako si yalikuwa wazi? Nakumbuka ukisema ulishuhudia.*

Noelah: Nilishuhudia ndio, lakini zimwi la kula

halizingatii hali halisi dadangu.

Dorah: Pole sana, ila mwachie Mungu. Siku moja mambo ya Ndwea yatamtobokea puani. Hakuna refu llisilo na mwisho. Kila safari ina tamati.

Noelah: Nasikitika sana kila nikumbukapo.... (*machози yanamlengalenga*) Mungu... Ilaze roho ya babangu pema peponi!

Dorah: Tuliza kasi ya machungu Noelah. Kumbuka kila siku ina mchana na usiku wake. Tena ukumbuke ili ardhi iitwe ardhi nyerezi lazima iwe na milima na mabonde. Ipo siku njiani yaja vituko hivi kwetu vitakuwa historia. (*Mlango unabishwa kwa kishindo. Wanaingia askari wawili kwa kasi*)

Askari 1: Tokeni! Tokeni!

Noelah: (*Kwa hamaki*) Nani? Kina nani? Msinikosee heshima tena. Hamjatosheka kwa hizo dhuluma mlizonipa?

Askari 1: Binti, usinipotezee muda wangu. Nasema ondoka!

Askari 2: Hatukuja malumbano. (*Anamjongea Noelah na kumshika mkono upesi. Noelah anaruka*)

Noelah: Mwataka kunipeleka wapi?

Askari 1: Unajua hili ni boma la wenyewe?

Askari 2: Chukua kilicho chako na utoke. (*Akimgeukia Dorah*) Wasikia?

Dorah: Hivi shetani wa mikono sita! Ni miaka mingapi Noelah na wazazi wake wameishi hapa?

Askari 1: Ni kauli ya mkubwa. Kauli ya mkubwa haitendwi kinyume. Atatoka atake asitake.

Noelah: Mkubwa ni nani?

Dorah: Mkubwa ni babuye Noelah, Marehemu mzee Msisi.

Noelah: Ambaye ni babake Ndwea na babangu Mkosi.

Askari 1: Hatuna haja ya historia za kina sijui babu wa baba wa nani.

Askari 2: Historia tuliacha shule.

Noelah: Wala haikuwabaki akilini?

Dorah: Iliingilia kushoto na kutokea kulia.

Askari 1: Tungeiweka itufaidi nini?

Noelah: Naona shani kubwa! Je, mtu husonga vipi mbele bila historia? Utajuaje uendako kama hujui utokako?

Dorah: Utajuaje safari ya kesho hupangwa leo? Kesho ifikapo leo itakuwa historia. Utategemea leo kesho.

Askari 1: Sasa ndio mnatuelimisha?

Askari 2: Tumekuwa wanafunzi wenu?

Askari 1: Mimi siwezi kuwa mwanafunzi wa vijitoto vichanga kama hivi. Haviwezi katu kuelimisha jamii

Dorah: Ni heri kwako hututambui, ila sisi wenyewe tunajua elimu ya jamii ipo mikononi mwetu. Kesho ya jamii kama hii ya Sarina inatutegemea kwa jitimai. Ni sisi, kama si sisi basi ustawi wa jamii yetu pia haupo.

Noelah: Na wala hatuoni huo mzigo kuwa mzito. Tunafahamu kuwa tufapo sisi vijana hatustahiki jina marehemu. Kesho ya jamii ndiyo inayoafiki jina hayati. Ndiyo maana tunashinda kumwambia mtemi kuwa ndiye anayeiangamiza jamii ya Sarina. Yumkini ameitia sumu tayari.

Askari 2: Unaona sasa ujinga wao? Ndio maana tunawaita viruka njia wambeya. Sumu gani anayoisema?

Askari 1: Achana na hawa wafidhuli. Sisi tunajua kwamba tunafanyia mtemi kazi. Tunafanyia serikali ya Sarina kazi.

Noelah: Eti nini...?

Dorah: Hii tena ni kazi?

Askari 1: Hatukujia maswali ya kipumbavu!
(Anamsukuma Noelah ambaye anaanguka chini kama gunia la viazi huku akipiga ukemi.)

Noelah: Yarabi! Mamaa...

Askari 1: Mama yupi?

Askari 2: Huyo ni maiti!

Dorah: *What...!* Eti nini?

Noelah: *(Kwa hamaki kubwa)* Mmemfanyaje mamangu?
Mmepeleka wapi?

Askari 2: Mtu mjinga hapaswi kuishi?

Noelah: Na msaliti je?

Askari 2: Hakuna msaliti hapa.

Askari 1: Hapa ni haki na amani.

Dorah: Kuwafanya watu yatima pia ni amani?

Askari 2: Amekufa! Amekufa leo asubui. *(Akiendelea kuwasukuma)*

Askari 1: Kipigo chetu si duni. Ni cha hakika! *(Vilio vinasikika hadi vinazimia. Taa zinazima taratibu.)*

GIZA

ONYESHO LA PILI

(Ndwea ameketi kwenye kiti cha mzunguko katika sebule ya jumba lake. Kando yake kuna viti kadhaa vya kifahari. Meza iliyoko mbele yake imezungushwa maua. Anazungumza kwa simu)

Ndwea: Salama... Vipi wewe na ndugu zako huko ng'ambo?... Huyu nimemaliza. Ameshazikwa... Mkewe nimefunga yuko ndani sasa hivi....Ndio, ndio, nimeshawambia askari wafanye kazi... Kabisa (*anacheka*)... Stakabadhi mpya ninazo... Hizo kamili zilifichwa... Hicho kisichana ... Nataka wewe upewe hiyo sehema. Ndio.... Naam. (*Unasikika mbisho mlangoni. Anazima simu na kuita*) Ingia. (*Anaingia Choche*)

Choche: Utukuzwe mtemi wa Sarina.

Ndwea: Amina. (*Anampa mkono na kumwashiria aketi*)

Choche: Asante, (*kimya*) nashkuru.

Ndwea: Vipi hali ya kazi?

Choche: Hamna cha mno. Kawaida kawaida tu.

Ndwea: Safi. Siku nyingi hufiki hapa.

Coche: Si mageni haya kwako. Nimelazimika kwenda mpaka mji wa Batu.

Ndwea: (*Anashangaa*) Batu mji mpovu bwanae.. si kwa

watu wa hirimu yako.

Choche: Lisilo budi hubidi. Huyu binti hashikiki. Alikuwa amekwamilia kabisa kivulana cha mama mjane.

Ndwea: Kisa na maana?

Choche: Eti kivulana kimepata elimu ya ng'ambo.

Ndwea: Haya makubwa kweli. Kina ajira kivulana chenyewe?

Choche: Wapi? Kitu hohe hahe. Kinafanya biashara sijui ya kuuza samaki kwa wazungu.

Ndwea: Huo ni upumbavu!

Choche: Nakwambia huyu binti yangu Vero anazidi kuniatua moyo kila uchao. Ni mwaka jana tu masomo ya shule ya upili yalimlelea akiwa amebakisha mwaka mmoja.

Ndwea: Nakumbuka ukiniambia. Sijui alitaka kwenda wapi vile.

Choche: Uarabuni. Ndio sababu nilimsukuma jela yule binti aliyetaka kumpeleka. Niliona amekosa kabisa kazi ya kufanya.

Ndwea: Ina maana kwamba hajui wewe ni lodi? Anakuona wewe kiumbe dhaifu usiyeweza kuwatunza wana wako?

Choche: Mwenyewe nipo tayari kuwashughulikia kila

mtu apate kazi.

Ndwea: Ndivyo hivyo. Lazima tuwashughulikie wana wetu. Hatuwezi ishi kitajiri na kuwaacha wana wetu kwenye ukata.

Choche: Naam. Vipi ile ya ofisi ya ubalozi wa nchi ya Sango?

Ndwea: Nadhani bado ipo. (*Kimya*) Lakini si wajua mtu huitaji cheti?

Choche: Hapo nitashughulikia. Najua namna ya kufanya.

Ndwea: Haya basi. Mipango ikikamilika mpeleke kwenye ofisi ya balozi. Umwambie nimeshaitikia.

Choche: Sawasawa. Asante.

Ndwea: Karibu. Wala hamna haja ya shukrani. Yetu huwa mamoja.

Choche: Ama kweli. Nashukuru pia umewaadhibu wahalifu.

Ndwea: Kabisa, walielekeza kidole kwenye shimo la nyoka. Kilichobaki sasa ni kupanga namna ya kukaribisha viongozi wenzangu. Lakini sijui nitatumia njia gani. Itabidi niumize mfuko zaidi.

Choche: Wewe nawe wataka pia kijiti kionekane mlingoti? Kitu kidogo.

Ndwea: Leta mpango.

Choche: Tumia askari.

Ndwea: Magaidi ni wengi. Hujasahau wakati ule tukipoteza askari?

Choche: Hilo lisikupe shaka.

Choche: (*Akizunguka kwenye kiti*) Ondoa shaka basi.

Choche: Ongeza idadi ya askari.

Ndwea: Hapo nitatumia pesa nyingi bwana.

Choche: Tuliza wasiwasi. Vitu ni mpango. Hujui mlo wa nyangumi na papa? (*Kwa sauti ya chini*) Ongeza karo ya vyuo vikuu na vyuo anuwai. Halafu upunguze pesa za mkopo kwa wanafunzi pia. Wanafunzi wa shule za upili karo yao iongezwe mara dufu kwa jina la kupanda kwa uchumi. Fedha zitaongezeka. Kwa hizo hizo fedha unachukua vipeni kuchani ukiwapa askari. (*Kwa sauti ya chini tena*) Mtu hula aajiriwapo bwana. Wataka ule wapi? Au wataka njaa ikumalizie hapa ulipo?

Ndwea: (*Akitikisa kichwa kwa maana ya kukubali*) Mwanzo hata huu mkopo unawapa wachochole mwanya wa kusoma kisha kuwavimbisha vichwa. Shahada moja inampa mtu kiburi cha kujilinganisha nami.

Choche: Ule mkopo wa kuwafadhili kwenda ng'ambo ung'olewe mara moja. Sioni faida yoyote ya raia wetu

kwenda ng'ambo. Ni sifa tu. Hazipikiki mekoni.

Ndwea: Lakini huu huwa ni mpango wa kimataifa. Wakija kosa kuwapata watanilaumu sana.

Choche: Acha kufikiria kilegevu! Ni kama mtu asiyejua kupiga hesabu.

Ndwea: Nifanyeje basi?

Choche: Wakileta pesa chukua weka kwa akiba yako. Kati ya wanafunzi kama elfu mbili waliofadhiliwa wewe peleka kama ishirini hivi. Labda wako ama wangu. Rejesha ripoti kuwa wengine wana matatizo labda ya kiafya. Wengine wakafariki kabla ya mipango kukamilika na wengine kukosa kuwa na stakabadhi za kutosha kwa sababu ya uzembe wao.

Ndwea: *(Anaagua kicheko na kumpa mkono tena)*
Choche...

Choche: Naam!

Ndwea: Wewe ni mrefu wa akili. Heko! Maarifa unayo kwelikweli.

Choche: Naam. *(Akicheka)* Nakwambia mlo ni akili mtu wangu.

Ndwea: Kweli kabisa. Nimeyaona leo.

Choche: Mtu huwezi kuishi kilegevu utarajie mlo

kushuka toka mbinguni. Hakujawai tokea na wala hakuwezitokea hata kwa tukizi.

Ndwea: Nakwambia fikra duni hazina tunda.

Choche: Tena ukumbuke mla ni mla leo. Mla kesho hata makombo hawezi kuambulia.

Ndwea: Haswa. Ngoja ngoja wanasema hufanyaje eti.

Choche: Haina msaada kwa matumbo. Huumiza tu. (*Kama aliyekumbuka kitu*) Ule mpango vipi...

Ndwea: Utakamilika, yuko kizimbani.

Choche: Naam, hatakuwa na budi ya kutaka kuokolewa. Tembo nitamwambia afikie hiyo nia. Mashairi yake nimeyaona magazetini ni mazuri sana. Yana mvuto wa aina yake.

Ndwea: Kama hili hapa. (*Akimwonyesha gazeti*) Ona jinsi alivyofafanua matunda bora wavunayo vijana kwa kuwatii wazazi.

Choche: Tena kaweka mada murua kabisa: **Mbegu Njema.**

Ndwea: Anasema kwamba utiifu wapatao wazazi kutoka kwa wana wao ni mbegu njema waliyopanda.

Choche: (*Kama anayemtazama mawazoni*) Huyo binti ni kitu bwana. Mali safi! Lazima awe mkwe wangu.

Ndwea: Ndio hayo sasa.

Choche: Nitampa Tembo kila kitu. Almradi ampate.

Ndwea: Usiniambie masurufu pekee. Wajua mabanati wa aina hiyo huhitaji wingi pia wa akili. Upevu wa kufikiria. Uzito wa mawazo. Lazima ajifanye anayo, ikiwezekana aandikiwe. Asifike huko akapotoka atafukuzwa kama jibwa.

Choche: Tembo namwamini.

Ndwea: Kweli kabisa.

Choche: *(Akiinuka)* Lazima niende nimjuze sasa hivi. Waambie askari wasimdhuru sana.

Ndwea: Sawasawa.

Choche: Haya kwaheri.

Ndwea: Kwaheri ya kuonana. *(Taa zinazima taratibu)*

GIZA

ONYESHO LA TATU

(Ndani ya kijumba cha kusubiria mashtaka, kijilango cha chuma kimefungika zaidi. Inasikika sauti nyororo ikiimba beti za shairi kwa machungu. Tembo anapokaribia kuingia anatumia ili kuisikiliza)

Sauti: Vipi niwe Marekani, muhadhiri wa chuoni

Niwe bingwa duniani, nishike zote pembeni

Hekima hadi pomoni, kama yule solomoni

Mbele na nyuma ni giza, zimwi kuimeza nyota

Heshimike limwenguni, bara zote duniani

Nikate kiu jangwani, nimlike baharini

Niwe joto msituni, na kivuli cha nyikani

Mbele na nyuma ni giza, zimwi kuimeza nyota

Binadamu wa machoni, siye yule wa rohoni

Mwanadamu hayawani, utu wake u nguoni

Arihami wamdhani, kumbe zimwi la miwani

Mbele na nyuma ni giza, zimwi kuimeza nyota

Dunia imo mbioni, shaka hazijulikani

Mavumbi kote hewani, nifiche wapi machoni
Kilio changu mbioni, anisikilize nani
Mbele na nyuma ni giza, zimwi kuimeza nyota

Wa mifuko mizitoni, wamoni mle ndegeni
Vipi wasikilizeni, sauti toka mwituni
Vipi wasikilizeni, sauti toka jangwani
Mbele na nyuma ni giza, zimwi kuimeza nyota

(Tembo anafungua kijilango na kuingia sauti inapozimia)

Tembo: Sauti tamu kwelikweli! Imelainika pasi hata nusu ya kona. Habari gani laazizi?

Noelah: *(Anasimama huku amemkazia macho)* Tembo aliyekujiza uwepo wangu huku ni nani?

Tembo: *(Akimjongea)* Noelah, samaki wa dhahabu hakaliki mafichoni. Mpenzi wangu nataka nikutoe hapa. Waonaje?

Noelah: Tembo, ya nini wajisumbua? Umekosa kazi ya kufanya? Kuwa kwangu hapa ni haki.

Tembo: Haki? Haki gani?

Noelah: Ni haki ya Ndwea niwe hapa. Wananchi wa Sarina kuteseka ni haki ya Ndwea.

Tembo: Noelah, hicho ni nini unasema? Mimi nimekuja nikufanye uwe salama. Nikuonjeshe asali unywe maziwa.

Noelah: Unionjeshe asali ninywe maziwa. Asali chungu? Maziwa yaliyomwagwa ndani sumu? Bin Choche mimi si hadaiki.

Tembo: Asali chungu? Tangu lini asali ikawa chungu?

Noelah: Nenda, nenda kamuulize Said A. Muhamed. Utabaini ukweli kwamba vitamu tamu vina sumu.

Tembo: (*Anacheka*) Eti vitamu vina sumu. (*Kimya*) Wapotea. Sikiliza nikwambie.

Noelah: (*Anamwekea macho huku mkono mmoja kiunoni.*) Uniambie nini muungwana?

Tembo: (*Anamjongea karibu zaidi na kumwekea mkono begani.*) Noelah, binti wa Mkosi bin Msisi. Msichana wa kipekee katikati ya midume. Pole sana kwa wale waume waliofia kwa maandamano chuoni. Ila kwa sasa yakini kuwa nakupenda. Nakutaka uwe wangu mpenzi, muhibu, unipe huba! Wewe ambaye nyumbani mwangu nitazima taa mwanga usizimike! Waridi langu Noelah! Mwenye unyerezi komavu. Ubavu wangu ulioumbiwa kando! Basi niunganishe. (*Kimya*)

Noelah: Tafadhali Tembo, malimwengu ya walimwengu

yameniwazimisha. Usinifanye

kichaa zaidi. Humjui Natija?

Tembo: Natija ninamjua. Ila yeye yuko ng'ambo. Atakufaa vipi? Hata mazishi ya ndugu zako hakuja. Tangu lini fimbo ya mbali ikamuua nyoka?

Noelah: Mbona isimuue? Hebu niambie.

Tembo: Mja humkuta nyoka katoroka.

Noelah: Wapotea mwenzangu. Umbali wa fimbo humfanya mja kufikiria njia gani mwafaka ya kumuua nyoka kiwepesi. Ya karibu hulazimisha pupa. Na ukumbuke, pupa ya fisi ilimfanya kuchomeka ngozi.

Tembo: Hivyo waamini chelea chelea ya Natija kutoka ng'ambo ina manufaa kwako?

Noelah: Ndio, huyo ndiye aliye na asali ya kweli na maziwa halisi.

Tembo: (*Anacheka kicheko cha kejeli*) Mtu asiyekuthamini. (*Kimya*) unadhani anakujua? Hakutambui wala. Tazama anakosa kutembelea ukiwa taabani. Ni misiba mingapi umekuwa nayo bila kumwona? Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

Noelah: Hilo si hoja. Natija alikereka kwa namna mambo yalivyo kwenda. Mtemi wetu alielekeza uzito wa nanga kwa

kifo cha askari mmoja Bwana Simbi ilhali wasaka taaluma kumi na tano waliokata roho hakushughulikia familia zao. Ishirini na tano waliojeruiwa walijiuguzia hospitalini. Walionafuuka walinafuuka waliokufa walikufa. Sijasahau taarifa zilizobeba mauko sita baadaye.

Tembo: Noelah, nawahurumia sana nyinyi wanafunzi mnaojiingiza...

Noelah: Mimi nilishapeka jina muhafala. Ninayo shahada ya utangazaji.

Tembo: Pole, kwa nini wanafunzi wanajiingiza kwenye siasa wasizozijua ndani na nje?

Noelah: Nasikitika yalikushinda. *(Tembo anaficha hisia za kukerwa)* Kawaida ya kitanda usichokilalia kunguni wake huwatambui. Wewe nikujuaye ungekuwa bado huko ungekuwa kiongozi wa maandamano kila mchana na usiku.

Tembo: Hayo si ya sasa. Turudi kwa mjadala wetu. Nataka nikutoe hapa shimoni ulipo upeperuke upae juu. Kesi hii nataka nikupe wakili akutetee usifungwe. Na pia ninao mpango.

Noelah: Mpango gani?

Tembo: Nimepewa nafasi ya kuwa mwenyekiti wa kamati

inayosimamia maandalizi ya wageni.

Noelah: Wageni wepi?

Tembo: Marais wa nchi zote za Afrika wameandaa gongamano la wiki moja. Litaafanyikia humu nchini. Mimi ndiye mwenyekiti wa kamati inayoendesha mipango.

Noelah: Kwa hivyo mnapanga nini? mmefikia wapi?

Tembo: Mambo mengi. Mwanzo nataka nikupe nafasi uwe msimamizi wa mawasiliano. Wanahabari wote watakaofika wakati huo wawe chini yako. Kwa ufupi sekta hiyo nakupa uisimamie. Nataka Nikutoe hapa upeperuke juu ya dhahabu.

Noelah: Dhahabu gani? Dhahabu iliyochomekwa ndani mikuki inidungedunge? Ni ning'inie juu ya hewa kwa machungu? Nibaki hohe hahe asiyeambilika wala kusemezeka? (*Kimya, anacheka kwa kejeli.*) Ndoana yako ni butu muungwana. Hiingiki hata chambo.

Tembo: (*Anaonekana kukasirika*) Noelah, wajua mimi ni nani juu ya maisha yako? Wajua ninao uwezo wa kukufinya kama nzi kwenye vidole vyangu? Nisikilize mdogo wangu, mimi ni mtoto wa naibu mtemi wa nchi hii ya Sarina.

Noelah: Wanihadidhia yanifae nini yale? Au yakufae nini

ukijitapa? Hongera basi. Kalifanye lolote ulionalo aula kwako. Nina imani siku moja mkono wangu utaliua zimwi lililomeza nyota ya Sarina.

Tembo: *(Baada ya kimya cha kubatini sana. Anautia mkono mfukoni, anautoa na kumsalimu kwa mara nyingine.)* Samahani Noelah, tuheshimiane. Sijakuja tuumbuane wala kuvuana nguo. Angaa nisikukoseshe amani nawe unipe heri zangu.

Noelah: *(Kama asiyejielewa)* Basi umekuja vema. Unatakaje?

Tembo: Haja yangu kwako waijua siku zote. Sijaanza leo wala sikuanza jana. Ikumbatie tuipe mipaka kwaheri. *(Kimya. Noelah bado hatamki. Anamjongea sana na kumkaribisha mkono mwingine karibu kumkuza.)* My dear.

Noelah: *(Akisonga nyuma hatua moja kwa haya)* Unasemaje? Si ujipe shughuli basi...

Tembo: Mapenzi yangu kwako hayaniruhusu kujipa shughuli nyingine kando na hii niliyojipa tayari. Juludi yako kama dhahabu yakomaza hanjamu zangu. Nawe jinsi ujuavyo kumpenda mtu si dhambi.

Noelah: Ndio, najua si dhambi.

Tembo: *(Akimvuta karibu sana)* Basi. *(Anavielekeza vidole*

kwa shavu la Noelah) Urembo wako unanivunja nafsi Noelah. (Anauteremsha mkono chini polepole kupitia kifuani kisha anaongeza ule mwingine huku kimya kimetawala. Mikono yote imefika kiunoni, wanatazamana pasi kutamkiana. Anaurefusha mdomo kuweka busu. Midomo inapogusana. Sauti inasikika katika mawazo ya Noelah)

Sauti: Tegemeo langu, dira yangu ya maisha, nakuaidi kutolivunja penzi hili. Kuwe giza kuwe mwanga, iwe gharika iwe kiangazi, yaje mawe zije pamba. Nitakuenzi daima. Mimi Natija ni natija yako. Penzi letu tulitunze kama mboni ya jicho. *(Noelah anashtuka mara moja na kumsukuma Tembo kwa nguvu. Tembo anajiokoa kufikisha uso chini kwa kutanguliza mikono.)*

Noelah: Punda milia! Kulungu! Pepo mchafu! Niondokee wewe zimwi! Unadhani. Nimesahau aliyoyafanya babako?

Tembo: *(Akiinuka)* Noelah, *(akijaribu kupiga magoti)* tafadhali ni...

Noelah: *(Kwa sauti kali)* Ni kome ulivyokoma la mamako!

Tembo: Noelah tafa....

Noelah: Nilishuhudia kwa macho yangu.... Walivyokuja Choche na Ndwea kwa nyumba...Wali... *(Anaanza*

*kurukaruka kiwazimu. Tembo anasonga karibu na mlango.
Noelah anaendelea kurandaranda huku akipiga mayowe.)
Baaaba.... Maaama! (Taa zinazima taratibu)*

GIZA

ONYESHO LA NNE

(Katika ofisi ya mtemi, anaingia mkuu wa sheria Bwana Toba)

Toba: Hujambo mtukufu mtemi?

Ndwea: Sijambo mkuu wa sheria. Habari za utokako?

Toba: Salama tu.

Ndwea: Jambo nililokuitia ni moja. Jinsi ujuavyo, ni lazima tujue ni wapi tunatoka, ni wapi tumefika na ni wapi tunakwenda. Kuna vipengele fulani kwenye katiba lazima viondolewe mara moja. Ya nini kitulacho kiwe nguoni mwetu?

Toba: Vipi hivo mtukufu?

Ndwea: Kipengele kwamba wanasarina wana haki ya kusaka taaluma ng'ambo kifutwe mara moja. Huku ng'ambo waendako kunanipa shaka fulani. Elimu ya Sarina ni tosha. Pili, haki ya wa hukumiwa kujitetea ifutiliwe mbali. Kisomo kingi kimevimbisha watu vichwa. Wamekuwa na uwezo wa kubadili ukweli uwe uongo na uongo uwe ukweli.

Toba: Sawasawa mkuu.

Ndwea: Jambo hilo nataka lianze kutetendeka sasa hivi.

Toba: (*Akibadilisha mkao.*) Kunradhi kiasi mtukufu; nasikitika haliwezi anza sasa hivi. Hadi mwaka kesho.

Ndwea: Kwa nini?

Toba: Kulingana na sheria zilizobadilishwa mwaka jana. Katiba histaili kuwekwa viraka katikati ya mwaka. Iwapo pendekezo lipo lisubiri hadi mwaka mpya.

Ndwea: (*Kwa hasira*) Mimi sipendekezi kitu. Zangu ni amri. Lazima zifwatwe, mtake msitake.

Toba : Ni kweli jinsi usemavyo mtukufu. Wewe ni mkuu lazima uheshimiwe. Kifungu 150 kilichowekwa mwaka juzi kinakupa mamlaka tosha ya kauli yako kutopingwa. Ila ni vyema tukipe kifungu 200 heshima tusichafue katiba katikati ya mwaka.

Ndwea: Hivyo hamwoni si jambo la busara kukiuka kifungu 150?

Toba: Mkuu, ikumbukwe kwamba hakuna kifungu kinacho kiukwa. Hakuna yeyote atakayeijadili kauli yako. Itawekwa jinsi ulivyosema. Heshima hiyo ndiyo tunayowekea kifungu 200 cha katiba hiyo hiyo.

Ndwea: Naona umeanza kupoteza busara.(*kimya*) Huna heshima kwa mtemi. Una kiburi ehe? (*Kimya*) Naomba ukiwa unazungumza na mimi, uwe na heshima na adabu

zake juu. Sawa!

Toba: Mtemi wa Sarina. Sioni kama kuna heshima niliyokuvunjia. Katiba ni kitu muhimu na ni lazima kipewe heshima zake. Hatuwezi kiuka katiba tuliyoibuni, pendekeza na kupitisha wenyewe. Huu ni usaliti tunaojisababishia wenyewe.

Ndwea: Ni mimi nimesema. Mimi ndiye mtemi wa nchi hii. (*Akipekua pekua kurasa kwenye daftari la katiba*) Kati yangu na hivi vijikaratasi ni nini muhimu?

Toba: Sheria ni kubwa kuliko mtu. Wewe ni mwana wa Adamu.

Ndwea: (*Kwa sauti kali*) Toba! Toba! Sikiliza nikwambie, wanasema heshima si utumwa. Niheshimu mimi mtemi wako. Nasema nipe heshima zangu!

Toba: Mtemi wa Sarina, heshima si utumwa ndio, lakini ni utumwa kama ni kulazimishwa kuheshimu kisichoheshimika.

Ndwea: Kwa hivyo mimi sisitahiki heshima. Ndio au la!

Toba: Mtemi, ni bora uelewa tofauti kati ya haya mambo mawili; heshima na uoga. Mtu akikuheshimu si kwamba atakosa kukuambia ukweli kwa lengo la kukutoa kwenye mvange unaokukodolea macho. Anastaili kukurekebisha

akuweke sawa, ubaki msafi kama pamba ndipo heshima izidi kudumu. (Kimya kifupi) Mtu mwoga hatakurekebisha ataogopa kukuambia ukweli. Mtaanguka shimoni nyote. Uoga si heshima ndugu yangu. Na ukumbuke, uoga ni kirusi kwa lengo la mtu.

Ndwea: Kwa hivyo wewe huniogopi? Huniogopi kabisa! Waweza pigana na mimi! Sio?

Toba: Sivyo nisemavyo, mtemi wewe vipi?

Ndwea: Vipi? Umesema mwenyewe hapa.

Toba: Bwana mtemi utakuwa mtoto mpaka lini? Unakuwa mwepesi wa hasira mno. Tuliza mori unielewe. Mimi sina haja ya kupigana na wewe. Tangu lini hili likatokea ofisini? Sasa mimi na wewe tukipigana hapa ofisini, machokora wenye kuranda randa kule mjini wafanyeje?

Ndwea: (*Anapunguza kusinasina*) Haya basi.

Toba: Jinsi nilivyosema, katiba hii si mswaada wetu. Ina husu wanasarina wote. Kumbuka yenyewe pia inasema iwapo swala lipo linalostaili kubadilishwa lihusishwe wananchi wote. Huwa tunafanya makosa tunapoyabalidilisha maswala fulani bila kuwahusisha wananchi. Mara nyingi tunajificha kwa kauli kwamba katiba isibadilishwe

katikati ya mwaka. Hapa wananchi wanatuona kuwa wema.

Ndwea: Hiyo ni kawaida yako. Hakuna kitu wewe unakosa kuweka dukuduku. Nani asiyekujua?

Toba: Ndugu mtemi, uongozi unahitaji kufikiria sana. Si kutenda kitu kwa sababu ya kutenda. La hasha! Kabla ya kuamua kutenda kitu jiulize wananchi hasa upande wa upinzani watachukulia vipi swala lako.

Ndwea: Lakini mimi sina upinzani. Wapinzani wote niliwamaliza.

Toba: Wewe wawachukulia hawa vijana kuwa kitu kidogo? Chunga sana wana mengi wanayoyafahamu. Kumbuka nyuki ni mdudu mdogo lakini humliza ndovu amwingiapo mkongani.

Ndwea: Kwa hivyo wewe wawapigia upatu watakuja kuniangamiza?

Toba: La! Nisemacho ni kwamba tucheze na akili zao kwa kujifanya kuwa wataratibu. Watakapo ligundua hili turudishe akili pamoja tuone lipi muhimu tena.

Ndwea: Haya basi, hata mwaka kesho si mbali.

Toba: Nawe uwe mwangu kuniita kila itokeapo dosari.

Ndwea: Nategemea sana Choche.

Toba: Almradi akusaidie.

Ndwea: Halafu ninawazo.

Toba: Lipi mkuu.

Ndwea: Kutokana na hitilafu hii kifungu 200 pia kitimuliwe. Mambo mengine ni ya dharura.

Toba: Sawasawa. Tutajadiliana kwa wakati halafu tuone.

Ndwea: (*Amekasirika*) Kujadiliana kujadiliana. Tutajadiliana mpaka lini? Jambo likisemwa litendwe. Hii mijadala ni ya nini? Ndio maana kila mara unashinda ukivurutana na wabunge. Unachukua muda mwingi kabla ya kuidhinisha miswada yao.

Ndwea: Mtemi; kondoo, mbuzi na ng'ombe huongozwa kwa amri moja tena kwa wepesi. Lakini binadamu ni kiumbe aliye na uwezo wa kubatini. Anajua kutofautisha baya na zuri. Kabla hujamwongoza unastaili kufikiria na kumfikiria kwanza. La si hivyo atakujua kabla hujamjua.

Ndwea: Unaona sasa hadithi zako?

Toba: Vipi?

Ndwea: Acha basi tutapanga jinsi usemavyo, umeanza kunipotezea muda.

Toba: Haya basi, una jambo jingine kabla niondokee?

Ndwea: Ndio.

Toba: Lipi?

Ndwea: Naamini umejiandaa vema kwa mapokezi ya wageni.

Toba: Ndio.

Ndwea: Tarehe haiko mbali. Andaa vizuri hotuba yako. Sitaki aibu.

Toba: Nimeshajiandaa.

Ndwea: Halafu naamini mahoteli yote yako sawa hamna mshike mshike ndani. Marais wasije wakavaamiwa na majambazi usiku.

Toba: Naamini mwana wa Choche atatudhibitishia hayo siku tatu kabla wafike. Uchachari wake ni wa kuaminika.

Ndwea: (*Akitabasamu*) Kumbe hatukukosea? Ndio maana huwaambia watu shahada ni tofauti kabisa na uchachari.

Toba: Kabisa.

Ndwea: Asante.

Toba: Una jingine?

Ndwea: Nimeota ndoto.

Toba: Ipi?

Ndwea: Kuna kidege nilikifungia nyayani, baadaye kikajiokoa na kutoka. Mjo wake wa pili hukuwa wa salamu. Kilinidungadunga macho hadi yakatoboka.

Toba: Kidege kimoja? Mbona usikitimue?

Ndwea: Kilikuwa na midege mingine ya mbawa za rangi ya kutisha.

Toba: Lo! Ulikiona kikikudunga?

Ndwea: La hashu. Hakikuonekana. Hiyo midege ndio ilikuwa imenisimamia. Kilipotokea wakati huu macho yangu yalikuwa yameseseleka zaidi.

Toba: Alaaa!

Ndwea: Wewe unaonaje ndoto hii?

Toba: Mimi sielewi kabisa.

Ndwea: Itanilazimu kutafuta mtafsiri. Maana pia mimi mwenyewe sipati lolote.

Toba: Ningekushauri hivo.

Toba: (*Akiinuka.*) Haya basi mimi naomba kuondoka.

Ndwea: (*Anampa mkono*) Haya kwaheri. Karibu tena

Toba: Nashkuru mkuu. (*Taa zinazima taratibu*)

GIZA

ONYESHO LA TANO

(Katika chumba cha wafungwa wa maisha, wafungwa wawili wamelala kifudifudi juu ya malazi kuukuu. Askari 2 ameshika bunduki mkononi anatembea tembea mle ndani. Anamwangalia mfungwa mmoja ambaye anatoa sauti nzito ya kugoroma. Anatia bunduki chini na kuchuchumaa alipo. Anamwita.)

Askari 2: Kombo... Kombo... *(Kimya)* mambo yako yalikwisha kwenda kombo. Sasa huna jingine. *(Kimya kinazidi kutawala)*

Noelah: Mama yangu!

Askari 1: Usiniite mama! Waniona na rinda?

Askari 2: *(Akimzapa kofi)* Hapa panakutosha sasa! Mjinga wewe!

Askari 1: Na umetukera na vishairi vyako!

Askari 2: Havina mbele wala nyuma.

Askari 1: Hustaili kupewa nafasi wewe! Uhuru wako ni hatari kwa watu wa Sarina!

Noelah: Laiti ungelijua usemalo.

Askari 1: Kwani ndiwe wa kwanza kuitwa yatima?

Noelah: Si mimi wa kwanza kuitwa yatima. Ni nani asiye

yatima Sarina?

Askari 1: Unaona sasa, amepandwa na wazimu.

Noelah: Afadhali niwe wazimu. Nisionekane mbele ya maasi yanayoendelea Sarina. Sarina nchi tuliyojivunia kuwa na rangi nyeupe na kijani kibichi, imekuwa nchi nyeusi tititi mithili ya giza la mvua na wekundu kukolea ndani.

Askari: *(Akicheka)* Sasa hajielewi kabisa. *(Anajaribu kumwita)* Binti mdogo, unajua ulipo?

Noelah: Sijielewi, mimi nimekubali. Nani anayejeelewa Sarina? Tungekuwa tunajielewa tungeitunza nyota ile tunayoizika. Mwanga wake angalau ungetufikisha pazuri.

Askari 1: *(Anacheka kwa kejeli)* No.. Noe.. *(Kwa Askari 2)* anaitwa nani vile?

Askari 2: Sijui Noha ama Noeea. *(Anacheka)*

Askari 1: Wewe Noha, hukumbuki hata katika Bibilia kauli za Noha hazikupendwa na watu? Ikiwa hiyo safina yake ilipuuzwa ilhali alikuwa mwanamume, sasa wewe mwanamke nani atakufwata?

Noelah: Lakini kumbuka hiyo Safina iliokoa walimwengu waliokubali kuingia ndani. Licha ya mafuriko yaliyousomba ulimwengu wote, Safina hiyo ilitua juu ya mlima Araret.

Askari 2: Huyo alikuwa mwanamume. Nawe mwanamke Safina yako itatua wapi?

Noelah: Hapa Sarina juu ya mlima Sarina. Tena wanasarina wote wataisikiliza na kuitii sauti yangu itakayolia kutoka mlima Sarina.

Askari 2: Ndio maana adhabu ya mwanamke hikutoshi wewe. Sijui unataka nini? Haikosi ulikuwa unawabeba waume sita kwa wakati mmoja huko chuoni.

Askari 1: Ndio maana ameharibika hivi. Hutapata wakukuo.

Askari 2: Na kama utampata ameshalaaniwa. (*Anamjongea sana*) Wewe... Wewe.. (*Anamzaba kofi shavuni.*) Sasa umefungwa maisha! Kumbe wewe muuaji! Katili!

Noelah: (*Akingeukia huku amelishika shavu*) Unajua mnyama ambaye anaitwa ng'ombe?

Askari 1: Ng'ombe wa kawaida sisi tunamfahamu.

Noelah: Sema wewe. (*Kwa askari 2*) Wewe unamjua ng'ombe?

Askari 2: Ndio, namjua. Amefanya nini?

Noelah: Tafakari. Unapotafakari ujitafakari pia na...

Askari 2: Nyamaza wewe ng'ombe!

Noelah: Umesema vema. Mimi ni ng'ombe nagoroma niletewe maji ng'ombe wenzangu nao wasisazwe.

Askari 2: (*Akipuuza maneno ya Noelah*) Amkeni nyinyi! Mbona mnalala mchana?

Mfungwa 1: Zima kelele nawe. Acha sisi tulale. Usingizi wetu unakuumiza wapi?

Askari 2: Acha ujinga wewe. (*Anapiga piga mfungwa 2 kwa miguu kisha anamkanyaga kichwa*)

Mfungwa 2: (*Akiwa bado amekanyagwa*) Aliye kwake wamwamshiani?

Mfungwa 1: Hata methali inasema alalaye usimwamshe.

Askari 1: Nani kawapa ruhusa ya kulala hapa?

Mfungwa 2: Nimesema hapa ni petu. Mtu ana haki ya kufanya jambo lolote akiwa kwake.

Noelah: (*Akiingia katikati ya wafungwa*) Hapa ni petu kabisa. Kumbuka Sarina ina jela tofauti tofauti.

Mfungwa 1: Na kila mtu Sarina ni mfungwa. Hata nyinyi askari ni wafungwa.

Askari 1: (*Anampiga kofi*) Kelele! Nakaa mfungwa mimi?

Askari 2: Zebe wewe! (*Anamwongeza teke*) Kombamwiko yonda.

Noelah: Jamani nawaambia! Kila mtu Sarina ni mfungwa. Walio na kazi kwa wasio na kazi. Walio gerezani kama sisi kwa walio nyumbani. Walioelimika kwa wasioelimika. Kila

mtu, yaani kila mtu.

Askari 2: Acha uwazimu nawe mwanamke. Kila mtu ni mfungwa hata mtemi?

Noelah: Kabisa! Yuko ndani ya jela ya kiu ya mali. Hana uhuru wa kushuhudia uhuru wa wananchi. Hii ni jela ambayo hatatoka mpaka siku ya mauti yake.

Askari 1: Acha ushenzi. (*Anamkaribia zaidi kwa hamaki*)

Naoelah: (*Akigeuka kumwonyesha mgongo*) Jela ya aina hii ni jela hatari kuliko jela zote duniani. Mtu amefunga roho yake. Kila faraja ya mtu ni sikitiko kwake. Kila uhuru wa mtu ni hangaiko kwake. Kila fanaka ya mtu ni huzuni kwake na kila neema humpigisha moyo konde. Mambo haya ulimwenguni ni maji ya mto usiokauka hata kwa kiangazi cha aina gani. Kujifunga ndani ya jela kama hii ni kujifunga kifungo cha maisha. (*Kimya kisha machozi yanaanza kumtoka*) Mtemi amewalisha majaji wanihukumu kifungu cha maisha! (*Kimya*) Afadhali mimi nimeona nikifungwa. Naziona pingu zangu. Ole wake yeye haoni mkufu mzito ulioizunguka roho yake ngumu!

Askari 1: Binti utaacha matusi. Mtemi wetu anapenda baraka kwa kila mtu. Ni nani asiyependwa na mtemi?

Noelah: Sasa hiyo ndio jela yenu askari pamoja na

wanasarina wengine. Mmefungwa jela ya kutoona maasi kwa waasi. Katili mnamwona malaika. Maovu mnayaona mema. Ila si walaumu sana, angalau jela kama hii mtu huweza kujikomboa pale zimwi lilomeza nyota yake lipatapo kuuliwa.

Askari 2: (*Kwa Askari 1*) Unamwelewa?

Askari 1: Wewe wataka kumwelewa wazimu?

Askari 2: Huyu si wazimu, tutafute jina la kumpa. Amepita kiwango cha uwazimu.

Noelah: (*Akigeuka kuwatazama*) Nipeni basi. Nipeni jina mtakalo. Mkikosa mniite Noelah binti wa Mkosi wa Msisi.

Mfungwa 2: Ukweli kabisa.

Askari 2: Wazimu wa kweli.

Askari: Hizi ni ngano zisizo na maana. Sielewi kabisa.

Noelah: Huwezi elewa. Maana minyororo iliyokufunga ni mikubwa na mizito mno.

Askari 1: Eti? (*Anamjongea zaidi kwa hamaki.*) Wasema nini?

Noelah: (*Anatazama ukutani*) Ndio, minyororo iliyowafunga watumishi wa mtemi ni nzito mno. Ni kubwa tena hatari mno. Imewashinda kuinuka. Imewashinda mpaka kusimama. Zaidi ya yote, imefanya macho yao kuwa

magumu kufunguka. Sasa hawaoni tena. Kwao yamekwisha!

Askari 2: Nilidhani kipigo kilikusaidia. Kumbe ujinga hujakutoka.

Askari 1: Na utakutoka. Utakutoka mama! Utakutoka!

Noelah: Ndio utanitoka. Lakini wenu ni uwele wa milele. (*Akiwageukia.*) Nawaambia hizi pingu mlizonifungia ni nyepesi kuliko uzito wa minyororo iliyowafunga ninyi.

Askari 2: Upumbavu!

Askari 1: Ujinga!

Noelah: (*Baada ya kimya*) Fungueni macho wanasarina.

Askari 1: Wewe binti, utachoka lini kulalamikia mambo yasiyokuhusu?

Noelah: (*Anamkazia macho*) Hayakuhusu wewe? Kwani wewe ni wa taifa lipi? Toka humo ngomeni ulimo. Inakuumiza nawe bado wajisitiri ndani.

Askari 2: Sitaki majibizano tena. Kaeni hapa na kelele zenu. (*Anaanza kuondoka*)

Askari 1: Zuzu nyinyi. (*Anaondoka pia*)

Mfungwa 2: (*Akimpa mkono*) Binti umeletwa kwa nini?

Noelah: Mimi ni muuaji.

Mfungwa: Wewe ni muuaji? Umeua nani?

Noelah: Watu wengi.

Mfungwa 1: Kina nani?

Noelah: Usiwe katu na hamu ya kujua. Hayatakufaa kivyovyote.

Mfungwa 2: Wewe ni mtoto wa nani?

Noelah: Mimi ndimi yule binti aliyekuwa kiongozi wa Chuo Kikuu Cha Sarina.

Mfungwa 2: Mwanamke wa kwanza kuwa rais *University of Sarina*?

Noelah: *Exactly. I was the one.*

Mfungwa 2: Ilikuwaje ukaua?

Noelah: Nimekupasha yale, mbona wataka kujua mengi?

Mfungwa 2: Inanishangaza msichana bado mbichi hivi unazalisha mauko!

Noelah: Itakushangaza.... Endelea kushangaa, ukimaliza ustaajabike.

Mfungwa: Acha kunizungusha mwanangu.

Noelah: Wewe waogopa kuzungushwa? Kwani wewe si mwanasarina? Unatoka taifa gani?

Mfungwa 2: Sikuelewi.

Noelah: Hutanielewa, maana mwenyewe sijaelewa. Sijaelewa kama mimi ni muuaji ama mimi ni mwokozi.

Mfungwa 2: Basi niambie kitu gani kimetokea?

Noelah: Ni kesi ya miaka mitatu kule nyuma. Niliua watu zaidi ya ishirini.

Mfungwa 2: Uliwaua kwa njia gani?

Noelah: Maandamano chuoni.

Mfungwa 2: Hujaniweka sawa.

Noelah: Ilikuwa baada ya wanafunzi kuwekewa gharama ya matibu vyuoni ilhali gharama yenyewe imejumuishwa kwenye karo, ndipo tulipoandamana.

Mfungwa 2: Nawe pia uliandamana?

Noelah: Niliongoza maandamano, askari wa mtemi wakaja kutuzuia ndipo vita vilipozuka kati ya askari wale na wanafunzi. Wanafunzi wengi walikufa pamoja na askari mmoja.

Mfungwa 2: Do! Samahani kwa misiba. Hapo nawe uliaua nani?

Noelah: Mtemi ameifufua kesi kwa kusema kwamba ndimi sababu ya vifo hivyo.

Mfungwa 2: Mbona akakufanyia hivyo ilhali watu wengi walimlaumu yeye?

Noelah: Ndio maana nikakwambia ukimaliza kushangaa ustaajibike.

Mfungwa 2: Makubwa haya! Kwani wewe ni mtoto wa nani?

Noelah: Mzee Mkosi.

Mfungwa 2: Mkosi? (*Anampa mkono tena.*) Mkosi wa mzee Msisi?

Noelah: Ndio.

Mfungwa : Una hakika kwamba wewe ni mtoto wa Mkosi

Noelah: Nina hakika.

Mfungwa 2: Una hakika ya kweli?

Noelah: Ndio, mbona huniamini?

Mfungwa 2: Sioni katu mshabaha.

Noelah: (*Akicheka*) Alaa... Kwani lazima tufanane?

Mfungwa 2: Ndio.

Noelah: Na ni vipi unamjua?

Mfungwa 2: Wala usijali.

Noelah: Ni lazima nijali. Wajua enzi hizi mtu kukufahamu ni jambo la kivyake kidogo.

Mfungwa: Kivyake namna gani?

Noelah: (*Akitabasamu*) Lazima pawe na la ziada mbali na huko kufahamiana.

Mfungwa 2: (*Aki tabasamu pia*) Wewe nawe una mambo. Nitakwambia.

Noelah: Hapana. Niambie sasa hivi. Tupo kwetu. Wataka uniambilie wapi?

Mfungwa 1: Kuna nini tena?

Mfungwa 2: Wewe nawe songa mbali. (*Anamsukuma*)

Mfungwa 1: Niwacheni basi nilale.

Mfungwa 2: Binti, mimi na Mkosi tulikuwa kitu (*anaonyesha kidole kimoja*) Matembezi yetu yalifanya tuambuilie vipendwa vya roho. Mkosi alifaulu kumweka wake wa roho ambaye nasikia...

Noelah: Usitaje tafadhali.

Mfungwa 2: Pole, nilisoma na Mkosi chuo kimoja katika mji wa Sarina. Japo sote tulikula mwande katika safari ya kazi. Mimi nikala pia mwande wa pili kwa kutopata jiko. Muhibu wangu alipoota uhai tumboni, nilituhumiwa kumbaka.

Noelah: Eti nini? Ulim...

Mfungwa 2: Ndio, alikuwa msomi huko chuoni mwaka wa nne. Mimi na Mkosi tulikuwa tumetangulia kuhitimu miaka miwili mbeleni. Samahani, unaitwa nani?

Noelah: Jina langu Noelah binti Mkosi.

Mfungwa 2: Naitwa Ben Kombo.

Noelah: (*Anashtuka na kumwangalia kwa makini sana*)

usoni. Kimya) Ben nani?

Mfungwa 2: Kombo. Mbona hivo?

Noelah: Si hoja, endelea. Alifanyaje huyo binti?

Mfungwa 2: Harakati zake za kunitetea ziliambulia patupu. Usemi ulikuwa mbakaji amemlungurisha binti wa wenyewe. Huu ni mwaka wa 25 tangu nianze kula hii kalenda.

Noelah: (*Kwa tabasamu*) Unasherekea jubilee ya kalenda (*anacheka*)

Mfungwa 2: (*Akicheka pia*) Ndio.

Noelah: Huyu mtoto umewai sikia kumhusu?

Mfungwa 2: Ndio.

Noelah: Jina lake ?

Mfungwa 2: Silikumbuki.

Noelah: Mbona hukumbuki? Niambie yuko wapi binti mwenzangu?

Mfungwa 2: Ni miaka mitano tangu niarifiwe kuwa amekiunga na Chuo kikuu cha Sarina kutaalumia elimu kama mwalimu wa somo la Kiingereza.

Noelah: Kongole kwake. Nani kakutaarifu?

Mfungwa 2: Aliyeniletea tanzia ya mauko ya mamake ndiye kaniambia hayo.

Noelah: Pole sana. Ila kuna mshabaha naona.

Mfungwa 2: Vipi?

Noelah: Umesema hujui jina la mtoto?

Mfungwa 2: Sio kwamba silijui, silikumbuki.

Noelah: Lakini ulikosea baba. Mbona tu kusahau jina?
Hapo si kwako.

Mfungwa 2: Najua kwamba si kwangu. Nimewekwa.
Nimefungiwa gizani kiasi cha kutoona tena. Macho
yasipoona masikio hayasikii na akili hazikumbuki.

Noelah: Lakini kichwa kiwapo gizani na nywele kuwa
nyeusi tititi akili husalia tu kuwa nyeupe. Haibadiliki
rangi katu.

Mfungwa 2: Kabisa.

Noelah: Akili ilifanywa kuwa nyeupe ili mtu afikirie
mambo meupe, safi, mawazo yasiingizwe doa. Hapa pa
kuwa gizani na kusahau jina la mtoto ulijikosea.

Mfungwa 2: Nikusahau labda kidogo tu mwanangu. Niwie
radhi!

Noelah: Afadhali nipo. Nitakukumbusha.

Mfungwa 2: Vipi?

Noelah: Dorah Kebya, binti wa mama Atela.

Mfungwa 2: *What!* Umelijua jina la mke wangu. Dorah

hilo jina la mwanangu.

Noelah: Namjua Dorah sana. Mshabaha kati yenu ni mkubwa mno. Shogangu wa kufa kuzikana. Hadithi hii aliwainidokezea huko shuleni.

Mfungwa 2: Mungu wangu! Noelah! Kumbe damu...(Anamjongea kisha wanakumbatiana .)

Taa zinazima taratibu)

ONYESHO LA SITA

(Katika ofisi ya mkuu wa sheria, kumepangika viti vitatu amekalia kimoja. Mezani kuna daftari kubwa la katiba. Amezamia katika luja. Anabonyeza simu nakuitia sikioni, Mlio wa mpigiwa unaita pasi ya jawabu. Anaitoa sikioni, anaitia mfukoni kisha unaduwa. Mara anaitoa mfukoni tena na kuitia mezani. Anasimama na kujinyoosha. Anatembea tembea mle ofisini bila mwelekeo kamili. Mara anapofika mlangoni mlio wa simu unaita. Anairudi mbio)

Toba: Helloo.... *(Sauti ya mpiga inasikika ikijibu)*

Sauti: Hello... Hujambo dadi?

Toba: Salama sana labda wewe. *(Anaketi)*

Sauti: Hali yangu shwari. Najua umenitafuta sana.

Toba: Ndio, nimekutafuta sana. Unaendeleaje?

Sauti: Salama tu labda wewe.

Toba: Sina neno. Vipi? Mbona huna uhusiano mwema na mtemi?

Sauti: Ni hadithi ndefu. Siku moja nitakueleza.

Toba: Mbona sio sasa? Nieleze tu.

Sauti: Nimesema ni hadithi ndefu. Nikianza kuisema labda nitakumalizia muda bure.

Toba: Wala usijali na hilo. (*Kimya*) Najua pana mazingira fulani yeye kuhusika kwa kifo cha babako. Wala nawe hufai kuingilia mambo yao. Kama mtoto mzuri uliye na ndoto njema. Unastaili kuyavalia njuga.

Sauti: (*Kwa kigugumizi*) Dadi... Dadi... Usichojua ni usiku wa giza. Ndio maana nikasema ni hadithi ndefu...

Toba: Samahani. Basi niambie. Yalikuwa mambo ya familia? Migogoro ya kawaida katika familia?

Sauti: Sivyoy. Dadi...(*Analia*) Da....di.... Nilishu....

Toba: Basi nyamaza... Pole... Mungu atakusaidia (*inatulia*) Niambie basi.

Sauti: Picha ya vituko vile naikumbuka kama leo. Sitawai isahau mpaka siku ya maziko yangu. Wala sidhani kama nitazikwa nayo maana haikosi kitoto ambacho bado hakijaumbika tumboni mwangu kilishuhudia.

Toba: (*Anapumua kwa nguvu*) Haa!

Sauti: Ulikuwa usiku, usiku uliolaaniwa! Usiku wa giza nene! Usiku wa mawingu mazito! Usiku uliokosa NYOTA! Usi....(*Anaanza kulia kwa sauti chungu na kubwa*)

Toba: Pole ... Pole... Nyamaza... Nyamaza basi...

Sauti: Nakwambia..... Babangu aliokotwa vipande... Mguu kando.. mkono kando... kichwa kando.

Toba: Pole.... Pole... Pole sana ...

Sauti: Ilikuwa baada ya wiki moja tangu vipande hivyo viunganishwe na kuzikwa, ndipo nilipokutana na ulimi katikati ya vibuyu nilipokuwa nikifagia....

Toba: Maajabu gani!

Sauti: Ilibidi mwili ufukuliwe tena. Kumbe babangu hakuzikwa na ulimi...

Toba: (*Anapumua kwa kasi na kwa sauti*) Haaa...

Sauti: Harufu ilikuwa ya kurarua pua lakini sikuihisi. Maajabu niliyokuwa nikishuhudia yalipiku.

Toba: Samahani! Samahani sana!

Sauti: Dadi... Kuna mengi yakusahau lakini yale hapana! (*Kimya*) Hapana!

Toba: Do! pole!

Sauti: Isitoshe! Watu huheshimu mila na desturi za kwao. Lakini kwetu sikuona.

Toba: Vipi?

Sauti: Ni desturi kwamba mume huzikwa na mkewe mahali pamoja. Ila mamangu alipouliwa sikuona.

Toba: Ilikuwaje.?

Sauti: Aliteketezwa.

Toba: Aliteketezwa?

Sauti: Ndio. Nilitamani nikitoka jela nipewe angalau jivu nilizike kando ya kaburi la mabaki ya babangu lakini sikufaulu.

Toba: Mbona?

Sauti: Baada ya kuchunguza zaidi nafahamishwa kwamba majivu yake yalitubwa ndani ya ziwa Sarina.

Toba: Wachawi wale!

Sauti: Eti walimfanyia hivyo kwa hoja kuwa ni mjalaana. Kwamba alipatikana kwa nyumba ya Sheki babake Sarah. Mtemi akamhukumu kifo cha kipigo na kuteketezwa. Kwamba uhusiono wao ndio uliomfanya amuue babangu.

Toba: Lakini mimi nilifahamishwa kwamba mamako alikuwa amepatana na wakili wa kuifufua kesi ya kifo cha babako.

Sauti: Huo ndio ukweli. Lakini ndivyo chatu afanyavyo akiwapata wana wa nyuni.

Toba: Hata hivyo pole kwa yote. Nakuhurumia sana binti wa sura na tabia nzuri kama wewe kuyapitia hayo.

Sauti: Nishapoa. Nina imani kwamba Rabana hajanisahau. Pole pia endapo nimekuharibia muda kwa hadithi za kishenzi.

Toba: Wala sivyo.

Sauti: Asante. Wajua nakuheshimu sana kwa wema ulionitenda. Nilitokea kukupenda na kukuenzi tangia siku ile. Mungu akubariki mpaka na kizazi chako.

Toba: Asante. Wala usijali. Ndio maana tuliumbwa. Tusiumbue bali tuumbe.

Sauti: Asante. Haya basi. Una jingine kabla nikuage?

Toba: Ndio?

Sauti: Lipi?

Toba: Heko kwa mchezo wako wa kuigiza! Ulikuwa wa mvuto wa aina yake!

Sauti: Asante!

Toba: Mchezo huo ndio ulioratibiwa kuigizwa mbele ya wageni!

Sauti: Asante! Wageni wenyewe watafika lini?

Toba: Karibuni tu.

Noelah: Karibuni mpaka lini? Nilitamani kuwaona.

Toba: Kwani haupo? Upo wapi sasa hivi?

Sauti: Nilikwisha safiri ng'ambo.

Toba: *What! (Anaanguka makalio yanafika sakafuni. Kimya kinatawala)*

Sauti: Hello... Hello...

Toba: Hello..

Sauti: Mbona hivo?

Toba: *Sweetie* mbona hivo tena? Hukukumbuka maagano yetu? Ukaamua kunipa asante kama za punda?

Sauti: Samahani dadi. Sina shaka ulielewa hali yangu. Msaada huu ulikuwa wa kupimiwa muda. Mwanzo hata korokoroni ilikuwa imeula vya kutosha.

Toba: *(Akijirudisha kitini)* Ila nilikuwa nimekuhakikishia ushwari wa kila kitu. Ukasahau mazuri yote niliyokutenda. Visa yako niliiba katika ofisi ya mtemi, hakuwa radhi kuiwachilia.

Sauti: Nashkuru sana dadi. Pole! Niliona haya kukupa ukweli wangu. Naomba nikueleze sasa hivi.

Toba: Eleza *(Anajiweka mkao sawa.)*

Sauti: Hakika ni kwamba nakupenda dadi. Wewe ni mtu kati ya wema wa ulimwengu huu. Na katika Sarina wewe ni mmoja kati ya milioni. *(Anavuruta miguu sakafuni)*. Una utu usio kifani. Kunipa Visa na kusikia kilio changu cha kumweka Ben Kombo huru ni kati ya mazuri ya kukukumbukia daima dawamu. Japo naomba nikupe fahamu kwamba mimi nimechumbiwa tayari.

Toba: Eeh! Unasema? Kwani mimi siwezi kuwa mchumba wako? Ninakosa nini cha kukuposa?

Sauti: Dadi, wewe huna ubaya. Ni wa adili na unyerezi pia. Lakini si wajua ndoa ina mambo yake?

Toba: Mambo gani yale nisiyoyafahamu?

Sauti: Umesema vema. Upo ndani ya ndoa tayari. Sio?

Toba: Ndio.

Sauti: Mkeo ni rafiki yangu sana. Namheshimu kufa yangu, naye ananipenda sana. Hunichukulia mwanawe. Si vema kuyavunja haya.

Toba: Hamtaishi pamoja. Wewe nitakununulia shamba lako, naye abaki kwa hilo.

Sauti: Samahani! Samahani dadi! Nawaheshimu nyote. Wewe na mkeo. Sitaki mambo ya kuvunjiana heshima.

Toba: Hakuna heshima itakayovunjwa. Mwanzo ndio tunaimarisha mahusiano.

Sauti: La hashu! Mimi kwa heshima zangu, hali yangu na udogo wangu siafiki katu kuona uchi wako. Huwenda nitapofuka. Wewe ni mtu wa heshima na adili zako.

Toba: Lakini nakupenda. Wewe ni mwangaza wangu.

Sauti: Hivyo una haja na mimi sana?

Toba: Ndio, tena sana. Nakupenda sana!

Sauti: Nami pia nakupenda. Tena sana. U kati ya watu nisiotaka kuwapoteza.

Toba: Basi tuungane tuwe kitu kimoja.

Sauti: Tulishakuwa wamoja. *(Toba anatabasamu)*

Toba: Basi ujapo utalikuta shamba na nyumba yako ndani.

Sauti: Hapana. Usijisumbue. Wajua ninacho maanisha kweli?

Toba: Kwani wamaanisha nini?

Sauti: Samahani. Nipo radhi kukupenda, kutendea yaliyomema, kukutakia kheri. Ila naomba unielewe kwa heshima ya ndoa yangu. Wakati wote shida zako ziwe zangu, zangu nazo ziwe zako huku misingi ya ndoa ikidumu.

Toba: *Baada ya kimya)* Sawa, utakuwa wangu mwandani. Wakati mwema.

Sauti: Pia nawe dadi. *(Toba anaiweka simu mezani, anajishika kidevu huku akifinya finya jicho moja. kisuguti cha mkono wa kulia kimekuza paja la kulia. Anainua uso huku bado kidevu amekishika. Mawazo yake yanasikika.)*

Toba: Mwanamke akizungumza hivi huwa ameridhia. Nitamfanyia kila kitu hata akaniambia nini.... Nina hakika atakaporudi atanipa muda hata kama ni sekunde moja kitandani. Noelah... Malkia wa ulimwengu!

(Anasimama, anafungua mlango na kutazama nje. Anarudi ndani huku mikono mfukoni. Analifunua daftari pasi ya kukisoma chochote. Anatingiza kichwa kwa namna ya kukubali. Anavua koti na kuliweka kititini. Anaketi tena pale kitini kisha wazo linamtoka) Noelah dhahabu ya dunia! (Taa zinazima taratibu)

GIZA

SEHEMU YA PILI

ONYESHO LA KWANZA

(Katika chumba cha Dorah, ameketi yeye kitandani huku Tito na Sarah vitini. Watatu hawa wamezamia soga huku wakiburudika kwa soda na njugu.)

Dorah: Nilihisi kufika kwenu.

Tito: *(Kwa Dorah)* Huku nje maisha namna gani lakini?

Sarah: Kweli tuambie. Kama kuna asali na maziwa tuje tuburudike. *(Kimya)*

Dorah: *(Kwa tabasamu.)* Mnangojea jibu langu?

Sarah: Ndio...

Tito: Hee...

Dorah: Mnatarajia nini mjapo huku nje?

Tito: Matunda ya jasho letu.

Dorah: Matunda ya jasho lenu ni nini?

Sarah: Ajira tena ya kipato kinono.

Dorah: Kanipeni sikio; magonjwa ya tauni, kipindupindu, malaria, pepo punda, yataje yote yale magonjwa hatari. Hayafikii gonjwa kubwa linalowasubiri nyinyi. Litawavunjavunja, liwabondebonde, liwatie kwenye kebe lililomo sumu ya bafe halafu liwatupe mwituni. Gonjwa

lenyewe mnalijua?

Sarah: La hashah!

Dorah: Ni gonjwa la matumaini. Ni jambo la kunikatisha maini sana kwamba nyinyi wanafunzi wa mwaka wa mwisho, tena viongozi wakuu wa chuoni hamfahamu hali halisi ya nchi yenu.

Tito: Dada, wewe ulihitimu mwaka jana. Sasa hivi unaitwa mwalimu. Mbona sielewi?

Dorah: Wapi? Tito, usiistaimilishe nyumba ya nyasi vishindo. Kichwa cha kuku hakistahiki kilemba. Mimi nimeajiriwa na bodi kuu ya shule. Nambari za walimu sina. Ikumbukwe kwamba wapo waliohafali miaka mitano kabla yangu bado kuzifikia hizo nambari.

Sarah: *Jesus christ! (Anautia mkono kwa shavu)*

Dorah: Uliza maiti adhabu ya kaburi uijue. Kuishi humu nchini ufuate mkondo wa nduma kuwili. Pande zote hufana mwendo wake. Nawambia ndugu mjapo huku nje muweni matopasi. *(Kimya kila mtu mkono kidevuni.)* Kumbukeni maprofesa ni wachoma mahindi, ni wachunga mbuzi, sembuse sisi wa shahada?

Tito: Lakini Dorah, kwa nini kampuni kubwakubwa zinawaajiriwa wasio hata na star shahada? Studio ya

hapa mjini ina mtangazaji ambaye hakuhitimu masomo ya sekondari. Kitu gani kinaendelea?

Sarah: Kuna wahandisi hapa nchini wanasimamia ujenzi wa barabara na magorofa hapa mjini ilihali taaluma zao ni tofauti. Wengine ni wanasosholojia.

Dorah: Nimeshawaambia jameni. Titi la mama likikosekana hata la mbwa huhamwa. Usisubiri kupewa kazi ya kisomo chako.

Sarah: Lakini hili ni tatitizo linalohitaji tiba. Inakuwaje mtu ametaalumia ualimu halafu aishie kufanya kazi benkini? Vipi? *Is he or she going to lesson plan there?*
Dorah come on!

Dorah: Hijakunyea mvua. Itakapoanza utakuwa wa kwanza kuiacha kazi ya taaluma yako na kufanya kazi nyingine tofauti kabisa.

Sarah: Usiniambie hivo! Usiniambie kwamba kila mara tutakuwa tukipoteza kiasi hicho.

Tito: Ina maanisha kwamba yote yatakuwa ni bure?

Dorah: Yote hayatakuwa bure. Angalau utapata cha kutia mfukoni kila mwezi na cha kutia tumboni kila siku.

Sarah: Kutia mfukoni na kutia tumboni hiyo wala si sababu ya ufanisi kwa taifa. Tunaangalia taifa limepiga

hatua gani kiuchumi au kimaendeleo kwa ujumla.

Dorah: Kwani hayo si maendeleo? Mtu kupata riziki ya kila siku si maendeleo?

Sarah: Si maendeleo hata! Nikuchanganyikiwa huko. Nani atalipa ushuru kama hajatambulika kwa serikali kwamba ameajiriwa? Au niulize. Au nikuulize, daktari ambaye ameishia kuwa fundi wa kujenga nyumba ataambia vipi serikali ameajiriwa na kwamba yuko radhi kuanza kukatwa ushuru?

Tito: Isitoshe, ni jinsi gani wakaaji wa nyumbani humo watakuwa na uhakika kwamba maisha yao hayamo hatarini ilhali wamejengewa nyumba na mtu ambaye si mhandisi bali daktari?

Sarah: Ndio maana nasema, nikuchanganyikiwa. Taifa lote limechanganyikiwa.

Dorah: Taifa limechanganyikiwa, tumlaumu nani?

Sarah: Tuilaumu serikali.

Tito: Tatizo limo serikalini!

Dorah: Tatizo la serikali. Jana tatizo serikalini, leo tatizo serikalini, kesho tatizo serikalini. Ni lini tutakubali kwamba pia sisi tuna matatizo? Kumbuka wale waliopo serikalini ni watu kama sisi. Wana mapungufu kama sisi.

Husahau na kukosea kama pia tufanyavyo sisi. Tusiwachukulie kuwa malaika.

Sarah: Tusiwachukulie kuwa malaika. (*Kwa msisitizo*) Na hatuwezi, labda wenyewe wajifanye malaika jinsi walivyojifanya tayari. Watu wasiorekepika, watu wasiosikiliza, watu wasiokubali mapungufu yao tusiwaite malaika. Tuwaite jina gani?

Dorah: (*Akimwangalia*) Dadangu Sarah, tufanye kazi. Tusionike, tushike majembe tulime mashamba yetu. (*Kwa Tito*) Tito..

Tito: Bee

Dorah: Kazi tuichape! Tutafute kazi, kazi haitujui wala haina haja ya kutujua hivyo haiwezi kututafuta.

Tito: Hivyo unamaanisha serikali ikifanya maovu tusiipinge. Hata wakiangusha kampuni zetu kubwa tusilalamike. Tutazame tu?

Sarah: (*Anahangaika*) Nashindwa la kusema. Nashindwa! Sijui Dorah karogwa ama nini. Umekula nini?

Dorah: Mmeshindwa kunielewa. Sio? (*Kimya*) Kwani nyinyi kule chuoni mnajifunza nini? *Or you are just after first class, aren't you?* Huku kushinda njaa mchana kutwa, wakati mwingine mpaka usiku hakumfunzi chochote nyie?

Sarah, hujui kwamba unastaili kuwa na hela zako? Hela za mkono wako. Hela za jasho lako?

Sarah: Ninajua. Ndio maana nilifanya bidii shuleni nikafika Chuo Kikuu ili nipate shahada niajiriwe, kazi inijazie ghawazi.

Dorah: (*Analazimisha kicheko*) Ndugu zangu, kitambo kabla ya kuzaliwa kwa kina bibi na babu zetu masomo hayakuwepo. Lakini palikuwepo na walitima na wenye nafasi. Tofauti ilitokea wapi?

Tito: Bidii ya mtu.

Dorah: Umesema vema. Bidii hiyo ilikuwa ya kisomo?

Tito: Hapana.

Dorah: Unasikia Sarah?

Sarah: Nakupata. Endelea.

Dorah: Nakwambieni ndugu wadogo zangu. Ingekuwa ni karatasi za mtu kumpa hela, Sarina kila mtu angekuwa na gari. Asilimia sabini ya watu Sarina wangekuwa na ndege. Pesa hazitafuti mtu bali mtu hutafuta pesa. Au ni nani kati yenu amekutana na pesa juzi zikamwakua jinsi alivyoziadimikia? (*Kimya*)Pasi ya marefu, ufanisi wako huanza na wewe mwenyewe wala sio serikali. Hapo tuelimishane.

Sarah: Kwa hivyo tuufumbie macho moto unaozichoma nyumba zetu?

Dorah: Sijasema hivyo hata. Mtu ana haki ya kukitetea kilicho chake. Kukosoa serikali sio vibaya. Lakini kosoa serikali ukijua baada ya mkutano huo wa kuonyesha ubabe wako jinsi ulivyo sugu wa kupingana na serikali, utarudi kunywa nini, utarudi kula nini, utarudi kulala wapi, na kesho utavalia nini. Hilo ni jambo la muhimu ambalo kila mwenye kuishi anapaswa kulijua.

Tito: Dorah usemavyo ni kweli.

Dorah: Najua, angalau nyinyi ni watu wa kuwajibikia maisha yenu. Lakini mbona tusiendelee na huo wajibu? Mbona tusikaze kamba mpaka kesho tutandike pesa tulalie. Kuliko kuendelea kuilaumu serikali bure.

Sarah: Wajua kitu ambacho huelewi ni hiki dadangu.

Dorah: Kipi? Sema Nakusikiliza.

Sarah: Ndio, tutawajibika, tutafanya kazi za mikono yetu kujijazia kipato chetu cha kila siku. Tutafanya kazi ambazo labda hata si taaluma zetu. Lakini mpaka lini hali hii? Mwenyewe huoni kwamba haya ni mambo ambayo hufanywa kwa sababu ya kuvumilia? Uvumilivu huu utaendelea kuwa vifuani mwetu mpaka lini?

Dorah: Nchi hujengwa na wananchi. Serikali ni kielelezo tu.

Sarah: Kama wananchi ni wakujenga nchi basi hawapewi nafasi waijenge. Inakuwaje baadhi ya mawaziri wa mtemi hawana shahada? Wapo walioingia vyuoni wakakosa kukamilisha kisomo. Vijana wengi huku nje na shahada zao hawana ajira. Ni kuranda randa tu.

Dorah: Hapo sasa! Kurandaranda tu. Mbona kuranda randa? Hiyo ni dalili ya kwenda shuleni kupita mitihani wala si kuelimika. Mtu aliyeelimika mpaka kufikia upeo wa shahada hawezi randa randa. Badala yake atajua cha kufanya kimmegee tonge.

Sarah: (*Kwa msisitizo*) Afanye nini ilhali serikali hijampa kazi?

Tito: Ni ufisadi tu. Watu hutafuta kazi zaidi ya miaka mitano bila manufaa yoyote. Dorah acha kutupumbaza.

Dorah: *Oh my God!* (*Kimya*) Sarah na Tito msiniambie mna ujinga kiasi hicho. Miaka mitano ipite tangu kuafali niwe sina hata senti! (*Kimya*) Kwani mimi ni mjinga kiasi gani? Hiyo ni shahada, karatasi iliyoandikwa jina la mtu, bongo bure.

Sarah: Eti...

Dorah: Bidii yako. Bidii yako ikutoe pale kwa ukulima wa mboga uwe meneja. Utatumia digrii yako, kufanya kazi yako, katika kampuni yako.

Tito: Naelekea kupatana nawe. Lakini kumbuka jukumu letu kupigana na serikali si la matumbo yetu tu bali ya wanasarina wote.

Dorah: Nami niliposema mjapo huku nje muwe matopasi si kumaanisha nyie wawili tu bali kijana yeyote anayatamani kuonja mwangaza wa nyota yake.

Tito: Tujishauri vipi basi?

Dorah: Imani ya kuamini kwamba serikali yetu ina apungufu haitatusaidia ama haitatutekelezea majukumu, ni uvivu wa mtu kuwajibika. Ni nani ambaye amewai tia chakula cha jasho lake mezani halafu mtemi akaja mwenyewe au akatuma askari wake wakaja kukimwaga? Isitoshe, kama kweli lazima kidole cha lawama kinyoshewe serikali yetu kutokana na ulitima unao tunasa, tunapaswa kujirudi tena sisi wenyewe. Kumbuka, sisi ndio wapiga kura.

Wale vijana ambao shahada zinaozea masandukuni mtawapata wakati wa kampeni wakiimba nyimbo za Ndwea.(kimya) Kama kweli sisi vijana tunaona kujenga

ukuta ni vigumu, mbona tusizibe ufa?

Sarah: Haswa!

Dorah: (*Kama aliyekumbuka kitu*) Tumesema mengi nikasahau kuuliza.

Mmefikisha wapi mipango?

Sarah: Ni sababu moja iliyotufanya tuje. Leo usiku tutakuwa na mkutano mtandaoni. Usikose.

Tito: Muungano una wafwasi zaidi ya elfu kufikia sasa.

Dorah: Heko! Na umeanzishwa juzi tu.

Sarah: Hata baada ya mwanzilishi kupewa kifungu cha maisha!

Tito: Kitu kizuri ni kizuri tu hata kikandamizwe namna gani.

Dorah: (*Kwa Sarah*) Nasikia ndiwe uliyepewa usukani.

Sarah: Ndio. Ulijuaje?

Dorah: Huwezi jua tulitoka wapi na Noelah. Tumeishi naye muda wote tangu alipotoka jela hadi aliponiaga akienda ng'ambo.

Sarah: (*Anashangaa*) Ala! Hakumjuza yeyote mahali alipokuwa.

Tito: Ndio maana ulishinda ukitusogezea mbele tarehe ya mjo wetu hapa?

Dorah: Hatukuwa tunaishi hapa wala.

Sarah: Kumbe mlikuwa mnaishi wapi?

Dorah: (*Akitabasamu*) Usiwe na shaka. Yalikwisha.

Sarah: Hata hivyo.

Dorah: Sasa unafanya kazi kuwili? Kama rais wa wanafunzi tena wa muungano?

Sarah: Naam! **Sarina Youth Association.** *Motto:* Pamoja tunakwenda mbali!

Tito: *Together far we go!*

Dorah: Yananikumbusha mchezo ule wa Noelah, uliigizwa jana kwa runinga ya **Tuelimishane.**

Tito: Nilliutazama jana. Kumbe ulihifadhiwa.

Sarah: Ulikuwa mtamu sana.

Dorah: (*Akimtazama Sarah*) Ndio uliofanya jumuiya ya Afrika kumtaka huru. Nawe pia uliutazama?

Sarah: Maigizo ya Noelah niyakose? Mwigizaji tajika? Kurunzi yangu? Aliupa mada

NYOTA. (*Akijaribu kuigiza*) Jameni! Tufanyeje ndani ya msitu huu?

Tito: (*Anaingilia maigizo hayo*) Giza nene limetanda. Limetanda mbele yetu.

Sarah: Tazameni ile nyota, ina mwanga halisi.

Dorah: (*Akirejelea uhalisia*) Kumbe mnajua. Katika mchezo huo binti mmoja anauwa kwa risasi.

Tito: (*Akirudi kitini*) Tena binti wa chuo kikuu! Ila ni bora zimwi linauwa na nyota kuchomoka ndani ikiwa na mwanga wote.

Sarah: (*Akiketi*) Mungu wangu! Angemwacha aione nyota yake iking'ara.

Dorah: Ulimwengu hukujui dada. (*Anasimama kuzikusanya chupa na vijikaratasi vya njugu.*)

Sarah: Turudie mjadala wetu. Vituko hivi ni sambamba na hali halisi ya nchi yetu. Hata sisi tuko katika msitu wa giza. Tunahitaji nyota. Ningekuwa mimi Noelah niandike mchezo huu, kiongozi huyo ningemuhukumu kinyongo cha kumteketeza hai mbele ya umati. Viongozi waafrika wasome, wazikome kasumba zao. Badala ya kuteketeza ndoto za watu wateketee wao wenyewe.

Dorah: Ila huo ni ulimwengu wa kubuni tu dadangu.

Sarah: (*Kama anayefikiria*) Do! Ingekuwa heri wanasarina tujue kwamba tulipoteza, tunapoteza na tutapoteza. (*Kwa Tito*) Ndio maana lazima tuseme na mtemi.

Dorah: Ila naomba kuwashauri.

Sarah: (*Anakuwa makini sana*) Vipi?

Dorah: Kabla ya kumfikia mtemi ningeomba mwanzo mmfikie mkuu wa sheria.

Tito: Mbona hivo?

Dorah: Atawafaa sana kumwelewa mtemi. Halafu kabla yake pigia Noelah simu akupe kina chake. Kuna jambo analifahamu kumhusu.

Sarah: Basi tutaanzia kwake asubui kabla twende kwa mtemi adhuhuri. Noelah nitasema naye usiku kabla ya mkutano.

Dorah: Haya basi, kila la heri!

Sarah: Asante. Nina imani kila mtu atakuwepo.

Tito: Mkutano huu utakuwa wa lengo moja. Kubadilisha Sarina. Tuliopo vyuoni tufanye kazi yetu, wale wa ng'ambo wafanye kazi zao, waliobahatika kupata kazi vile vile.

Dorah: Nguvu pamoja tuisake nyota. Bora nyota yatosha.

Sarah: Hatuna jingine, ni hiyo tu.

Dorah: Haya basi na tumtangulize Maulana.

Tito: (*Akiangalia kwenye saa.*) Sarah, muda umeyoyoma. Bora tuondoke huwenda tusipate gari la kuturudisha Chuoni. Si unajua hali ya hapa mjini mida ya jioni?

Sarah: Mwanzo misongomano ya magari huwa wimbo wakati huu wa jioni. (*Akiinuka kitini*) Dorah, shukurani

sana kwa muda wako. Tupatane mtandaoni *zoom*.

Dorah: Ila nitawakosa sana. (*Anawakumbatia kila mmoja*)
kwaheri, Safari njema.

Sarah: Na utuajiri tukufanyie biashara. Sijui vipi wafunza
pamwe na kufanya biashara.

Dorah: Kazi rahisi tu. Nawe mboga ulimwachia nani
nyumbani? Tito najua ndugu wanamsaidia mradi wa
kuku.

Sarah: Mzee Sheki na mwamini.

Tito: Wala hawafanyi kazi ya kutosha. Ila Alhamdulilahi.

Sarah: (*Huku bado wanasalamiana.*) Tuonaneni jamani.

Dorah: Karibuni tena wakati wote.

Sarah: Asante

Tito: Ubaki salama nawe. Asante. (*Taa zinazima taratibu*)

GIZA

ONYESHO LA PILI

(Katika ofisi ya Mtemi wameketi Tito na Sarah kwenye viti vilivyo karibu na mlango. Askari wawili wamewasimamia. Mmoja upande wa kushoto mwingine upande wa kulia. Kimya kimetawala. Kwa mbali kidogo sauti ya mlio wa ndege aina ya bundi inasikika. Vile vile kwa mbali zaidi sauti ya mwanamke asiyejulikana inasikika ikiimba wimbo wa kuomboleza. Mlio wa sakafu kuumizwa na vyatu unasikika kutoka upande mwingine, Kisha anatokea Ndwea upande huo huo.)

Ndwea: Hamjambo wajuzi wetu? Karibuni. (Wanaviendea viti vya katikati karibu na kiti cha mtemi.)

Tito: Mbona umetuweka sana?

Sarah: Mpaka salamu zako zinanuka!

Ndwea: Samahani waangwana. (Anawapa mkono kila mmoja) Mna yepi?

Tito: Hatuna majibu ya swali letu.

Ndwea: Majibu au jibu? Mlitaka nini?

Sarah: Tuliuliza maswali au swali?

Ndwea: Elewa Kiswahili binti mdogo. Sentensi ya wingi ikamilike kwa wingi umoja vile vile. Unanipata?

Sarah: Umejua lini Kiswahili? Sasa hivi wewe ni mhadhiri

wa Kiswahili? Eeh, (*Anapiga makofi huku akilazimisha kicheko*) Yaani siku hizi vibogoyo wanaguguna mifupa.

Karibuni viziwi watanunua radio kusikiliza habari, vipofu wanunue runinga watazame habari nao bubu watusimulie hutoba kwa ndimi zao.

Tito: Sarah, tunapoteza lengo. Mtemi tunataka majibu. Yawe ni maswali au swali.

Ndwea: Swali lenu ni lipi?

Sarah: Usianze kufumbia macho. Hukupata waraka wowote?

Ndwea: Nyaraka ninazo nyingi.

Sarah: Umejukumikia upi?

Ndwea: Sina muda.

Tito: Unamaanisha hujasoma? Mbona ulitukubalia tuje?

Ndwea: Kusoma nimesoma.

Sarah: Halafu?

Ndwea: Hujanipendeza. Maswali yenu ni ya upuuzi. Hayo hampaswi kujua.

Sarah: Mbona?

Ndwea: Hiyo Sentensi ya mwisho ya waraka sijui ilisema vipi vile. (*Anajaribu kukumbuka*) eeh, *Ex.... Explain in... not less than one thousand sentences the need for constitution*

change.

Sarah: *You have to.* Utake usitake.

Tito: Upende usipende.

Ndwea: Upuuzi!

Sarah: Upuuzi? Mwenye upuuzi ni wewe!

Ndwea: Nafanya kazi yangu kama mtemi. Nilipigiwa kura na wanasarina wote. Tena niliapishwa mbele ya umati mkubwa. Hamtaniambia cha kufanya nyie watoto mlio bado na upwapwa shingoni.

Tito: Kwa hivyo watuona sisi wakembe. Sio?

Ndwea: Hamjafikia hata kuwa wakembe, hamjazaliwa bado. Maana hamjaona wala kuonja chochote duniani. Tulieni, ketini pale niwafundishe ulimwengu ulivyo.

Sarah: Utufundishe namna ya kufyonza pesa za umma? Kutumia jina la nchi kufanya mikopo kwa manufaa yako?

Tito: Kula na vibaraka wasio na elimu kichwani? Kufinya na kukanyaga haki za wanyonge?

Sarah: Utufundishe sisi haya maasi?

Tito: Ndiyo mihadhara uliyobobea?

Sarah: Utastaarabika ama utastraarabishwa?

Ndwea: Fanyeni mwonalo jema. Enyi wana wa nyuni vipofu.

Tito: Ndio, sisi wana wa nyuni. Nyuni uliowapofusha.

Sarah: Ukakata mti wao mkuu. Wasiwe na pa kujenga wala pa kutua. Ulipotea. Kumbe uliwakomaza hawa wakembe wa nyuni mapema.

Tito: Wamejifunza kuila mizizi ya mti ulio karibu na jumba lako. Chunga mti huo utaanguka usiku.

Ndwea: Nyinyi vijana mna ujinga! Hamniheshimu kama mtemi wenu. Hivi vishahada mnavyovisaka vimewafanya mvimbe vichwa? Mnajua kwamba mimi nina shahada ngapi? Mnajua nimefika wapi kielimu? (*Anasimama kwa hamaki*) mnajua nina vyeti vingapi? Hee? Kila mara ni migomo, migomo, inawafaidi nini hiyo migomo? Haswa nyinyi wanafunzi! Inawafaidi nini? (*Akigonga meza*)

Inawafaidi nini nauliza?

Sarah: (*Anasimama mkabala naye nakumnyoshea kidole*) Mori zako hazitauzima moto tuliukwisha uwasha. Wewe mwanzo tuambie una shahada ngapi? Unadhani hatujui kilichotendeka? Shahada za halali ni za marehemu Mkosi bin Msisi. Tuambie hizi zako ni za wapi?

Tito: (*Akisimama*) Hukuwa na sababu moja ya kumuua Mkosi. Mbali na kulinyakua shamba lake, alikuwa amemenyana na wachunguzi wa masomo yako. Tuambie

hao wachunguzi walienda wapi kama hukuwatia mfukoni. Na utujuze pia ni vipi shahada za Mkosi zilipotea.

Ndwea: Wajinga nyinyi! Pumbavu! Mmeshindwa kusomo mnachunguza mambo ambayo hayawahusu. Msijaze susu kwa yasiyo wa husu. Mtasusuwaa. Ni hivyo mnawatia wengine kwa mambo wasiyohusika. Noelah alikwisha ondoka nchini. Mbona mnamuhusisha kwa mambo yenu. *Akiangalia karatasi iliyochapishwa.*) Ni yeye aliyeandika barua hii. Ndilo hili jina lake.

Sarah: Pilipili usiyoila nawe yakuashia nini? Sisi tunaheshima kwa watu wote. Wawe wanafunzi, raia waliomo nchini au hata ughaibuni wote ni muhimu.

Tito: Si kama wewe unayewalenga watu wengine. Unawaona takataka ya juzi.

Sarah: Mzee tupe jibu la waraka wetu. Naona tunaelekea kwingine. Kwa nini unataka kubadilisha katiba? Katiba si kitu cha kubadilisha badilisha jinsi utakavyo.

Tito: Huo si wasifu wako unaondikwa bado.

Ndwea: Sijabadilisha katiba yote. Nimebadilisha tu vipengele fulani.

Tito: Kwa nini hutaki watu kutaalumia ng'ambo? Wewe huoni kuwa ni njia moja ya kijifunza mengi. Kuelewa

namna ya kujiendeleza kupitia kwa wengine.

Ndwea: Elimu ya Sarina ni tosha. Tunajiweza sisi wenyewe. Haina haja tena kuwategemea wale watu weupe. Kama ni maarifa tunayo. Wapo wahadhiri kutoka huko ng'ambo ambao tayari wamo humu nchini. Kama ni kutamani kufundishwa na mzungu wamo humu nchini!

Sarah: Elimu ya Sarina ni tosha.... Matatizo ya akili fupi. Huna soni wewe. Hutazami mbele. Fungua lile pazia nene liliyofungika mbele ya juso lako. Ni lini utapevuka wewe? Elimu ya Sarina inakuwaje ya kutosha ilhali wahadhiri wenyewe hawatoshi tunalazimika kuomba wengine kutoka ng'ambo?

Tito: Wale tuliowaona wanatosha mliwaachisha kazi kwa madai kwamba serikali haina hela za kutosha kuwalipa. Nashangaa ni vipi mnalipa wazungu.

Sarah: Wahadhiri wachache vyuoni. Shahada za uzamili na uzamifu mnataka tufanyie humu humu. Yatawezekanaje?

Ndwea: Shahada hizo zinaweza patikana tu hapa. Ni nyinyi wenyewe msiotaka kusoma. Kumbuka mshoni hachagui nguo. Tena mchagua jembe si mkulima.

Tito: Tungekuwa hatutaki kusoma tungetetea swala la kutaalumia ng'ambo? Wewe sema hutaki kugharamika.

Ndwea: Ni nyinyi msiotaka kusoma. Mmeanza visingizio eti mtemi sijui nini... Nilijua hizi mbio za masomoni sijui yamekuwa ya bure zitaishia ukingoni. Ulikuwa moto wa karatasi ambao kawaida haudumu. Ona sasa yamekuwa yale ya mbaazi kukosa kuzaa kusingizia jua.

Sarah: Wewe hukupenda elimu ya bure iliyoletwa na mtangulizi wako. Historia zinasema ukiwa mjumbe wa eneo bunge la Batu hukupenda sana mswada huo upitishwe bungeni.

Tito: Uliongoza hata maandamano ya kupinga katiba hii. Ndio maana unaibadilisha kama ngua zako.

Sarah: Na ukumbuke tunajua mara ya kwanza kuingia ofisini ulitumia milungura mingi kumwaga damu nyingi.

Tito: Kwa mfano, kifo cha Teti, ambaye alikuwa mfwasi sugu wa mpinzani wako wiki moja kabla ya uchaguzi mkuu.

Sarah: Isitoshe, ilikuwaje tu mpinzani wako alikufa wiki mbili baada ya uchaguzi? Kesi ambayo alikuwa amepeleka mahakamani ya kupinga uchaguzi huo ilikwenda wapi?

Ndwea: Acheni Mambo mengi wanangu. Mnajua nchi inatarajia wageni hivi karibuni.

Mbona mnataka kuleta machafuko mbele ya wageni?

Tito : Hatujali. Tunataka Sarina mpya! Nasikia eti kileleni mwa gongamano unapanga kusherekea miaka ishirini na tano ya utawala.

Ndwea: Mbele ya viongozi wenzangu. Niwaonyeshe matunda niliyoleta Sarina.

Sarah: Matunda gani? Matope ama matunda? Kwa taarifa yako, hiyo siku ya wageni kuwasili ndio siku tutazindua muungano wetu wa **Sarina Youth Association**.

(Kwa sauti, Tito akijibu) SAYA!

Tito: SAYA!

Sarah: SAYA!

Tito: SAYA!

Ndwea: *(Kwa hasira)* Enough! Mnashida gani nyie watoto? Mnajua mnacho kifanya? Mnajua naweza kuwafunga kwa kunipaka tope kubwa kiasi hicho? Washenzi nyinyi!

Sarah: Nenda! Nenda kotini. Sikiliza, *I know everything!* Niko na *first hand information*. Sisemi nisichokijua. *(Anamjongea karibu na kugeuka)* Hebu niangalie vizuri.

Aliyekuwa Naibu chanzela wa **Chuo Kikuu Cha NYOTA** alikufa kwa kulipuliwa risasi kwa sababu alikuwa na idhibati kamili ya chanzo cha mauti ya mpinzani wako.

Unajua zilipo hizo idhibati? Umezitafuta miaka mingapi?

Tito: Naye Choche mliyempa nafasi ya marehemu, alikifikisha wapi hicho chuo?

Ndwea: *(Huku akimsukuma)* Kimya! Kimya wewe mwanamke! Aliyewapa ruhusa wanawake mzungumze ni nani? *(Sarah anaanguka vitini)* Tazama katika serikali yangu. Unaona mwanamke ndani? Enzi zetu wanawake hawakuwa wanahusika katika vikao! Unasikia?

Sarah: *(Akiinuka vitini)* Mjalaana wewe! Sikiliza nikuambie pwagu! Kisa kwamba mimi ni mwanamke nimevaa sketi haimaanishi kwamba sijiwezi. Wanawake tunajiweza. Tupe nafasi uone kama hii ardhi hatutaifikisha mawinguni kwa sekunde moja. Usione wembamba wa reli gari moshi hupita.

Ndwea: Unaona sasa. Ameanza kuropoka. *(Zinasikika kelele nje ya ofisi)* Comrades power.. Power! Comrades power.. Power. Comrades SAYA... SAYA! comrades SAYA... SAYA!

Tito: Na bado. Haya mabavu yako hayakupeleki mahali, akili yako ni tepetevu.

Ndwea: Hizo kelele zenu ni za chura tu.

Sarah: Wakati unakuja zitakuwa za zilizala.

Ndwea: Hamna heshima, huo waraka wenu sitaushughulikia ng'o! Mnataka kwenda ng'ambo kufanya nini?

Sarah: Wewe mwana wako alienda kufanya nini?

Tito: Wala hakuelimika. Angekuwa alielimika angetofautisha halali na haramu.

Sarah: Yaani ajue shamba apokezwalo si halali ni haramu. Elimu pasi vitendo vya vya kielimu ni bure.

Ndwea: *Shut up!* Sitaendelea kuvumilia haya! (*Anatoa ishara kwa askari. Askari wanawajongea*)

Sarah: (*Huku amefura uso na mwili unatetemeka*) Nipige! Nipige! (*Anamtazama askari usoni. Askari anashika bunduki. Mtemi anamwashiria kuirudisha chini. Tito anamshika Sarah mkono kumvuuta nyuma.*) Utajua uume ni suruali tu!

Tito: Ndwea, huyu si mwanamke mojawapo wa wale uwaletao hapa kila usiku.

Sarah: (*Machozi yanamtiririka huku malaika yamemsimama*) Hajui jinsi ya kushughulikia haki zao! Kazi ni kuwageuza geuza tu vitandani! (*Kwa sauti ya juu zaidi*) Kumewaka Ndwea! Kumewaka hakuzimiki!

Ndwea: Huu ni moto wa karatasi. (*Ameanza kubonyeza simu*) Subiri siku mwanamke atakuwa mtemi ukatoe huo

ulimi wako nje au ukutomeze kwa bahari ya mchakoge.

Sarah: Kumbuka Ndwea; ulibebwa na mwanamke tumboni miezi tisa. Kwa wakarimu wa ulimwengu yumo Mather Theresa ila kwa hayawani wa ulimwengu Ndwea amebeba bendera yao. Nasimanzika sana moyoni! *Our country is almost becoming a failed state!*

Ndwea: Ropoka yote. Yako ni ya mdomo vyangu ni vitendo. *(Sauti zinazidi kusikika) We gooo we go... We go! We gooo we go... We go (sauti ya mmoja inasema huku wengine wakijibu. Ndwea anatazama kwa simu halafu anawaashiria askari waondoke. Ndani kuna kimya nje kelele zinazidi kuongezeka. Wanaingia askari wengine watatu tofauti.)*

Sarah: Hata uongeze idadi ya askari kiasi gani; hunitishi! Nitasalia kuwa Sarah binti Sheki kiongozi wa wanafunzi wa Chuo kikuu cha Sarina. Haki itandendeka chini ya Muungano wa SAYA! Utake usitake.

Tito: Mkuu haki tunayong'ang'ania si ya wanafunzi tu bali ya wanasarina wote. Huo ndio uungwana. Haina haja wengine kuteseka huku wengine wanasitirika. Kumbuka ndugu zetu wanaokufa kwa sababu ya njaa, ajali barabarani kutokana na ubovu wa barabara, ukosefu wa

tiba mahospitalini, haya na mengine mengi hufanya familia nyingi kuhangaika sana.

Sarah: (*Ametulia kiasi*) Watu wanauza mashamba, ng'ombe, kondoo, mbuzi, kuku na hata kila kitu cha nyumba ili wana waelimike. Mwishowe wanarudishiwa majeneza na kubakishiwa vijilima vyekundu mbele ya vijumba! Jivishe hicho kiatu!

Tito: Jitimai zaidi inatokea kwamba hata baada ya nusura ya mahangaiko haya ya chuoni, shahada yako inabaki tu sandukini. Kampuni zimeanguka, talanta hazikuzwi tutapanda mti gani sisi vijana wa Sarina!

Ndwea: Mmeyesema hata kwa barua ila mimi simtumi yeyote kwa mambo ya siasa. Na ha... (*Anaangalia kwa simu anashtuka, kimya, kelele bado ziko nje wakati huu zimezidi sana. Anamgeuza Sarah upande wa mlango na kumtamkia kwa hasira, macho yake ni mekundu*) Basi nenda kawaokoe wenzako!

Sarah: Kuna nini kwani? (*anamtazama Tito*)

Tito: Nini? (*Mlio wa risasi unalipuka nje. Vilio na mbio za kutafuta usalama zinasikika. Sarah anamvuta Tito mkono*)

Sarah: Twende, Tito twende (*Ndwea anamsukuma aende. Anauwacha mkono wa Tito kisha anasonga mbele kwa*

kasi. Ndwea anacheka. Tito anamfuata nyuma huku akiita.)

Tito: Sarah... Sarah... *(Sarah anafika mlangoni anapokutana na Askari 1 ambaye anamwelekezea mtutu. Macho ya Sarah yanaangaza zilipofanyika sarakasi. Anapiga ukemi. Risasi linalipuka. Sarah anaanguka chini. Tito anapomfikia nyama nzito inatokea mgongoni. Kabla hajainama kumshika, Ndwea anamvuta nyuma kwa nguvu. Anaushika mwili wa Sarah na kusema)*

Ndwea: Mavumbi kwa mavumbi majivu kwa majivu.

Tito: *(Anainuka na kuufikia mwili tena anautazama na kuukuza, kisha anatazama hadhira)* Tamaa ya mwili izidishapo malimwengu ulimwenguni dawa ni wajibu wa moyo. *(Machozi mengi yanambubujika usoni. Taratibu taa zinazima)*

GIZA

ONYESHO LA TATU

(Katika chumba cha kulala cha mtemi, amelala chali kitandani, mkono mmoja kipajini huku magoti yameinuka. Anajizungumzia.)

Ndwea: Ni vipi mganga alikosa kuelewa ndoto hii? Kidege... Kidege tu... Kinatoboa macho ya jitu la miraba minne kama mimi? Haiwezekani kabisa. Mimi niliyebingwa, ataniangusha nani? Yawe makonde mimi bingwa, kurusha mkuki mimi ni bingwa, kulenga shabaha mimi ni bingwa, hata utawala mimi ni bingwa. Jimwili ninalo. *(Analiangalia jimwili lenyewe)* Kidege hiki ni cha nini? Au ilikuwa ndoto tu? Mganga yule nina mwamini. Tena nilimpa ukweli hapo kilingeni. Tena ukweli wote. Ndio... Ndio... Nilimwambia nini hasa? Mmmh. *(kimya. Picha ya yaliyotokea inajitokeza jukwani).*

Mganga: *(Sauti inasikika katika kijumba cha msonge)* Mburrrrr! Haaaaaa! Hahahaaaaa Mburr Haaaaa! *(Inajirudia rudia kabla kutokea mtu. Mtemi anapotokea mlangongoni anasimamishwa)* Kinyumanyuma! *(Mtemi anasalimu maagizo)* Vua koti *(Mtemi anavua, bado yautembea mwendo wa nyuma)* Vua shati! *(Mtemi*

anawajibika upesi) Suruali isionekane! (*Mtemi anabakisha bombo*) Funga macho kisha uketi upesi! (*Anamsogezea jiwe jeusi. Mtemi anajibwatika.*) Mburrurr! Mpampam! Mburrurr! (*Anasimama wima na kumtazama mtemi*) Sema shida yako.

Ndwea: Papa mkuu wa wakuu, jua na mwezi viko chini yako! Kilichonileta....

Mganga: Rudia usemi wako kwa utaratibu.

Ndwea: Mtukufu wa watukufu...

Mganga: Huna unachoelewa. Simama wima!

Ndwea: (*Akiinuka*) Ndio papa.

Mganga: Ruka mara moja moja kila baada ya sekunde.

Ndwea: Naam papa.

Mganga: Haya *one.. (Anaruka) one...(Anaruka)* Huelewi kitu. Hebu rudi nje.

Ndwea: Ndio papa (*Akiondoka*)

Mganga: Fanya mbio!

Ndwea: (*Baada ya kimya kirefu akiwa nje*) Nakusikiliza papa! Nifanye nini?

Mganga: Umeharibu! Hukustaili kuzungumza mpaka dakika kumi ziishe.

Ndwea: Samahani!

Mganga: *(Kwa sauti nzito) Kimya! (Mtemi anasimama wima kabisa. Mikono yote imelainika kwa mwili. Kimya kinazidi kutawala. Baada ya dakika kumi.) Ruka wima mpaka mlangoni.*

Ndwea: *Asante. (Ananza kuruka)*

Mganga: *Usiseme chochote. Wala sauti isikutoke! (Anaruka ruka hadi mlangoni. Mganga amesimama wima kwenye ukuta wa nyumba. Wanatazana.) Ingiza mkono wa kushoto kisha wa kulia mwili ukiwa nje. (Mtemi anawajibika) Tia kitako chini na ufanye vile vile miguu. (Mtemi anawajibika) Rudia maneno haya baada yangu. Ndimi huyu wakuu.*

Ndwea: *Ndimi huyu wakuu*

Mganga: *Nimekuja na mizigo.*

Ndwea: *Nimekuja na mizigo.*

Mganga: *Basi njooni.*

Ndwea: *Basi njooni. (Sauti kali ya radi inasikika. Mtemi anaanguka kichwa kinatoka nje ya nyumba. Mganga anatetemeka mwili halafu anatingiza kichwa huku akiguruma.) Huuuuuu! Huuuuuu! (Anamfikia mtemi na kumuinua. Mtemi anapofumbua macho anaonekana kushtuka.)*

Mganga: Inuka mtemi wa Sarina.

Ndwea: (*Anahema*) Ni...nini... Ni... Niko wapi?

Mganga: *Huuu....* Usijali mtemi wa Sarina. Tupo hapa kwangu.

Ndwea: (*Anaanza kutingisha kichwa kama anakubali*)
Ndio... ndioo... Ndi...ndioo.

Mganga: *Huuuuuu....* Mtemi wa Sarina. (*Anamkalisha jinsi alivyokuwa mwanzo. Mikono na miguu yote imelainika kuingizwa chumbani. Huku mgongo waonekana nje ya nyumba. Anaziendea rangi zake na kuanza kumchora usoni, mikono na hata miguu. Anaanza kugonga vyombo vyake huku akiruka ruka kichumbani. Ha! Ha! Ha! Mburrr! Mburrr!*)
(*Kimya*) Mtemi wa Sarina nena shida yako!

Ndwea: (*Kwa sauti ya kitetemeshi*) Papa wa mwezi na jua!
Wanyama na mimea vyote wakusadiki! Nilikuwa usi....

Mganga: Hiyo ndoto nimeiona; hahahaaa! (*Akiinua mkono huku amefunga macho*) Kidege kilicho na macho kama nyota kinamluka mtemi wa Sarina. Kinatua miguu kifuani kwanza, kinaruka na kunyaga miguu kwa pua ya mtemi, kinaweka kinyesi baina ya midomo ya mtemi. Kijidomo kama sindono inafanya nini? Huuuuh! Haaah! Unahitajika kuwa na mbuzi mwekundu, kuku mweusi, ukucha wa

mamba na ulimi wa kinyonga! Utavipata vyote?

Ndwea: La hasha! Sina ukucha wa mamba na ulimi wa kinyonga.

Mganga: Basi hutaweza kusaidika.

Ndwea: Tafadhali nipe njia ya kuvipata.

Mganga: Una dhambi nyingi. Umemwanga damu nyingi! Umekandamiza roho nyingi! Umechafua akili nyingi! Akili nyeupe umezitia rangi nyeusi! Tatizo lako laitaji hivi vyote. La si hivyo unaangamia!

Ndwea: Hata uongozi wangu?

Mganga: Wala huna historia tena. Ukuu wako hutamithilika hata kwa maisha ya nzi! Maana vivuli vya familia ulizoangamiza vinakulia.

Ndwea: Vinasemaje?

Mganga: Naona giza mbele yako, naona giza nyuma yako, naona giza kando yako. Ulimwaga mpaka damu yako mwenyewe! Hapana cha kuridhi tena. Sarina yaitaji damu mpya uongozini (Anacheke)

Ndwea: Itakuwaje?

Mganga: (*Huku akitetemeka*) Tazama nyota inakuja. Nyota safi. Nyota iliyo na mwanga kamili wa kumlikia wanasarina. Hapatakuwa na giza tena. Mwanga halisi

unakuja.

Ndwea: Unaletwa na nani?

Mganga: Tazama, mwanamke maskini atakufa! Damu yake itatiririka kwenye viganja vya mikono ya mtemi wa Sarina. Itaririka mpaka kifuani. Damu hii ndicho itakacho kuwa kichocheo kikubwa cha balaa. (*Kimya kirefu*) Tazama mwanamke yatima anashuka toka milimani, ndiye nyota halisi ya wanasarina.

Ndwea: Sikuelewi.

Mganga: Hutaelewa. Maana mimi pia sielewi. Ila naona mambo makuu ambayo yatapata kujiri katika taifa la wanasarina.

Ndwea: (*Kwa sauti ya masikitiko*) Wala Sarina haihitaji ukombozi! Tulipata ukombozi zamani. Tumehesabu miongo sita tayari.

Mganga: Ukombozi unaitajika.

Ndwea: Vipi ilhali wanasarina walishakombolewa.

Mganga: Ukombozi mwingine unaitajika. Wanasarina wamefungwa kwa minyoro mieusi. Damu yao ikafyonzwa na majoka meusi.

Ndwea: Majoka? Majoka tu. Kunao watu wazito sarina wa kuyaua majoka yale.

Mganga: La hashah! binti yatima atalipiga joka kuu kwa mkono wake. Wanasarina wote watapumua. Lakini tayari litakuwa limemeza binti wa fukara.

Ndwea: Nami nifanyeje kama mtemi?

Mganga: Umezungukwa na giza nene. Macho yako hayataona tena.

Ndwea: Unanifanyia shere. Sindio?

Mganga: La hashah! Nakwambia ninayo yaona. Wala sikudanganyi lolote. Mkia wako umekatwa. Aliyekutazama hakutumia macho!

Ndwea: Vipi? Si macho ndiyo hutumiwa kutazama.

Mganga: (*Anacheka*) Mazimwi ya siku hizi hayatazamwi kwa macho. Mashujaa walishagundua. Wanatumia akili.

Ndwea: Basi nisaidie. Nifanyeje nijizuie kwa hili hangaiko.

Mganga: Sina namna. Nimeliona likijiri.

Ndwea: Wala hapana cha kuzuia?

Mganga: Cha kuzuia ni kile nilicho kuagiza.

Ndwea: Wala sitavipata vyote. Nisaidie jinsi ya kuvipata.

Mganga: (*Anaendelea kuguruma*) Mpaka kwenye nchi ya Ndolo. Semesha mwenzangu kule. Uwe na kitita kinono. Utasaidika. Ufanye upesi.

Ndwea: Asante. Nitafanya upesi.

Mganga: Kisha urudi kwangu.

Ndwea: Nashkuru.

Mganga: Haya inuka. (*Mtemi anainuka.*) Simama wima. (*Mtemi anawajibika, mara radi linapiga kwa mara nyingine. Wakati huu mtemi anajikuta kajipinda miguuni pa mganga. Mganga ametazama juu anaguruma*) Huuuu! Huuu!

Ndwea: Haa! Haa! Hee! Hee! (*Anaanza kujaribu kuinuka*)

Mganga: Salia pale ulipo. Naona pana kitu unataka kusema. Sema nakusikiliza.

Ndwea: Ta...tafa....Tafadhali. Ni wewe nategemea! Nisaidie kwa mambo haya sasa.

Mganga: Unataka nini?

Ndwea: Sitaweza kufika nchi ya Ndolo kwa wakati. Nifanyie msaada. Nifanyie kwa deni.

Mganga: Naitaji kitita kikubwa. Una hela ngapi?

Ndwea: Million hamsini!

Mganga: Kidogo sana. Ongeza mara dufu!

Ndwea: Nitaongeza mkuu papa yangu uliye hai!

Mganga: Leta. (*Mtemi anaanza kutafutisha mikono pale chini. Mara anainuka na kuanza kuitafuta suruali. Anaifikia na kuchopoa kibeti mfukuni. Anafungua na*

kutoka vitita viwili vya punda, ana mkabithi mganga. Mara anaanza kusikia mwasho machoni. Anajifukutua mfulululizo hadi anapoanguka miguuni pa mganga tena. Haya yakiendelea kwake, mganga anahesabu hela alizopokezwa. Anazitia kwenye kinu. Na kuutia mkono wake juu ya kichwa cha mtemi.)

Mganga: Utawala wa Sarina unaanguka mikononi mwa jinsia tofauti.

Ndwea: Niokoe papa!

Mganga: Hayo ndiyo ninayoona.

Ndwea: Yafute papa!

Mganga: Tuone iwapo wakuu watakubali kwa fedha ulizotoa.

Ndwea: Ndio papa!

Mganga: Wakuu pokeeni hela!

Ndwea: Ndio! (Akitetemeka) ndio papa!

Mganga: Huuuuh:

Ndwea: Ndio papa!

Mganga: Huuuh!

Ndwea: Ndio papa!

Mganga: Wakuu wanasemaje?

Ndwea: Ndio papa!

Mganga: (*Kwa hasira anamzapa mtemi kofi*) Kimya! Kimya wewe! wakuu hawapendi kelele za sauti geni. (*Mtemi anajikunyata zaidi kwa lile jiwe*) wakuu... (*Kimya*) Wakuu...(Kimya) wakuu...(Kimya) Mtemi wa Sarina? (*Kimya. Anaita kwa sauti huku akimongoa kichwa*) Mtemi wa Sarina!

Ndwea: Ndio papa!

Mganga: Ondoka urudi baadaye. Wakuu hawasemi. (*Mtemi anaanza kuvaa nguo.*) Ziwache nguo hapa. Nenda jinsi ulivyo wakuu wakuone ndani. (*Mtemi anaondoka*)

Ndwea: Hee! hee! hee! (*Sauti hii inaendelea mpaka anapojikumbuka. Anashtuka kiasi cha kuruka toka kitandani hadi mlangoni. Anapinduka pinduka mle chumbani huku akijiangalia kuhakikisha kama kweli ni yeye na kama kweli pale alipo ni pake. Taa zinazima taratibu.*)

GIZA

ONYESHO LA TANO

(Ndani ya ofisi ya mtemi, Choche na Toba wameketi kwenye viti. Toba ameegemea kwenye kiti na kutazama upande unaokinza na Choche. Choche naye ameinama chini akiwa ametia mikono kwenye magoti. Kimya kimetawala. Choche anainua kichwa na kutazama Toba)

Choche: Bwana Toba, mbona umekawia sana kufika katika mkutano huu?

Toba: Mkutano huu mwanzo una maana gani? Mbona mtemi akasema na wanafunzi kabla ya sisi?

Choche: Atakuja utamuuliza.

Toba: *(Akijiweka mkao sawa)* Ameleta ripoti gani kutoka kwa mganga?

Choche: Ndio maana ya mkutano huu.

Toba: *(Akisimama)* Mara baada ya kuua?

Choche: Tusubiri basi ripoti.

Toba: Kila mara arudipo kutoka huko huongea nasi kwanza kabla ya mtu mwingine. Iweje alianza na wanafunzi? Halafu mbona kumfanya hivyo huyo binti? Sijapenda!

Choche: Hivi kifo cha Sarah kimekuhatua sana? Eeh! Mwanzo nawe utuambie katika mkutano wa leo; kila mara mazungumzo yako na Noelah yana nini?

Toba: Hayakuhusu ndwewe wala sikio.

Choche: Nayo pepe aliyokutumia juzi ilikuwa na ujumbe gani? (*Anaingia mtemi*)

Ndwea: Hamjambo ndugu zangu? (Kimya) Kuna yepi?

Toba: Hatujambo. Hapana la mno mtukufu. (*Anasimama kumpa mkono, Choche anafanya vile pia*)

Ndwea: (*Akiketi*) Haya basi. Karibuni, (*Kwa Choche*) Wapi kijana? Anafaa atusomee ripoti ya mipango leo.

Choche: Alisema atakawia kidogo kwa sababu ya mishe mishe, japo atafika.

Ndwea: (*Kwa tabasamu.*) Hapana tatizo alimuradi afike.

Toba: Hapo ni sawa.

Ndwea: Nitamsimamisha mbele ya viongozi wenzangu kama kijana shupavu wa kuenzi maendeleo. Nataka viongozi waafrika wajionee jinsi nchi ya Sarina inavyokuza kesho ya vijana kwa kuwahusisha katika ujenzi wa nchi.

Choche: Ni fursa nzuri ya kuonyesha nafasi ya vijana katika jamii. Nadhani watajifunza kwamba si kila jambo la kuendesha nchi linahitaji wazee. Wapo vijana machachari pia wa kuendesha mambo.

Ndwea: Kabisa! (*Kama aliyekumbuka kitu*) Sina hofu ya usalama katika yale mahoteli kubwa.

Toba: Hapo nina hakika. Sijaona mshike mshike karibu na FURAHA HOTEL.

Ndwea: Vipi pale WEMA HOTEL? Ndugu Choche?

Choche: Hapana utashi wowote.

Ndwea: Nashukuru sana. Hii ni dalili ya ushwari wa mambo! (*Akibadili mkondo wa gumzo.*) Ila kama bado tunamsubiri ningependa tulizungumzie hili swala ambalo limeanza kujitokeza kivingine.

Choche: Lipi tena?

Ndwea: Nasikia watu wameanza kuandamana.

Choche: Kina nani?

Ndwea: Kila mahali, si walimu, si madaktari, takriban wafanyakazi wote wa umma.

Toba: Hali itarudi shwari. Bora tu...

Ndwea: Vipi wewe? Mwanzo tuambie kwa nini unataka kujiuzulu?

Choche: *What!* Unataka...

(*Askari 1 anaingia akihema.*)

Ndwea: Vipi? Unaingia bila hata kubisha! Kwani hapa ni kwako?

Askari 1: (*Kama ambaye hajasikia chochote.*) Mtemi una wageni wameshuka kutoka uwanja wa ndege.

Ndwea: *(Kwa wasiwasi)* Wamefika wapi?

Askari 1: Hapa nje, tuliwaongoza na wenzangu.

Ndwea: Ni kina nani?

Askari 1: Siwajui ni wazungu.

Ndwea: *(Anamtazama Choche. Choche kichwa hakiinuki)*
wambie waje. *(Askari 1 anaondoka huku Toba akimfwata.*
Wanaingia wazungu wawili na askari mmoja mzungu.
Mara waingiapo sauti inasikika mawazoni mwa mtemi)

Sauti: Tazama binti maskini atakufa. Damu yake
itamwagika kwenye viganja vya mikono ya mtemi wa
Sarina. Itatiririka mpaka kifuani. Itafufua damu nyingine
iliyowai kumwagika Sarina. Damu hii ndicho kitakacho
kuwa kichocheo kikubwa cha balaa kwa mtemi.

Mzungu 1: U hali gani mtemi wa Sarina?

Ndwea: Salama mkubwa wangu. *(Anawasalimu wote kwa*
mikono miwili. Askari mzungu hasalimiki. Choche anawasalimu
pia)

Mzungu 2: Habari ya wanasarina.

Ndwea: Hawajambo. Karibuni! *(Anawaashiria viti waketi)*

Mzungu 1 na Mzungu 2: Asante. *(Wanaketi)*

Ndwea: Poleni kwa safari! Karibuni sana hapa Sarina!

Mzungu 2: Asante!

Mzungu 1: Asante sana bwana mtemi!

Ndwea: Basi furahini mandhari ya hapa Sarina. (*Kimya kirefu. Anaashiria kwa Choche*) huyu hapa ni naibu wangu. Jina lake ni George Choche.

Choche: Naam.

Mzungu 2: George Choche. Nafuria kukufahamu.

Choche: Asante.

Mzungu 1: Nafuria kukujua pia nami bwana Choche.

Choche: Asante. Nami nafuria kuwajua enyi wakubwa wetu. Huwa nawasikia tu leo nimewaona.

Ndwea: Yupu mkuu wa sheria ambaye ameondoka sasa hivi tu. Ameitwa kwa mkutano wa dharura na wanakamati wa ofisi yake. Ofisi yake ni karibu kilomita mbili kutoka hapa. Yupu Bwana Matapo ndiye waziri mkuu. Yupu Bwana Shibe, msimamizi wa kitengo cha ulinzi. Nadhani yuko katika harakati za kupambana na ushwari wa mambo. Ofisi yake kidogo haijakuwa na mshikil hivi karibuni. Hata hivyo vitengo vyote vya serikali vinazidi kupiga hatua nzuri.

Mzungu 1: Asante. Ni vema kusikia hivyo.

Ndwea: Viongozi wengine wanashughulikia maandalizi ya kesho. Gongamano la viongozi wa nchi za Afrika

litafanyikia hapa Sarina kuanzia kesho.

Mzungu 2: Pongezi sana! Nafuria kusikia hivo. Hiyo ni hatua kubwa!

Choche: Asante!

Ndwea: Asante sana. (*Wote wanapiga makofi*)

Mzungu 1: Vema.

Ndwea: Vipi hali ya kule ng'ambo?

Mzungu 2: Huko kuna ushwari kabisa. Tunajaribu sana kuona maendeleo bora katika jumuiya ya mataifa ya Afrika.

Mzungu 1: Ni furaha yetu kuona mataifa ya kiafrika yakiimarika kwa kasi.

Choche: Huku labda janga lililotupa changamoto kubwa ni hili la virusi vya korona.

Ndwea: Kabisa. La si hivyo tungekuwa tumepiga hatua kubwa sana kuliko hapa tulipo.

Mzungu 2: Hata hivyo misaada ilifika?

Ndwea: Ilifika tena kwa wakati.

Choche: Shukrani sana.

Mzungu 2: Karibu.

Mzungu 1: (*Baada ya kimya*) Bwana mtemi labda utujuze kuhusu maendeleo ya kampuni tulizoanzisha kwenye nchi hii kama kitega uchumi.

Ndwea: (*Anaficha haya*) Ziko sawa. Zote zinaendelea vizuri. Watu wamepata ajira.

Mzungu 1: Hesabu iliyo kwenye mizani yetu ni kwamba nchi hii inastaili kuwa na kampuni kubwa 315 ambazo zinafaa kuzalisha uchumi wa taifa kwa asilimia sitini. Hilo ni kweli?

Ndwea: Ndio.

Choche: Ndio kabisa.

Mzungu 1: Mizani pia inaonyesha kwamba kampuni ambazo bado zina uhai ni kumi pekee. Tano kwenye mji mkuu hapa Sarina, tatu kwenye mji wa Batu kusini mwa nchi na mbili kwenye mji wa Samba magharibi mwa nchi. Kweli si kweli?

Ndwea: (*Kwa sauti ya kitetemeshi*) Ndio ila...

Mzungu 1: Ngoja kwanza bado tunaendelea. Inasemekana kampuni hizi zinazidi kudidimia kwa kasi kwa sababu ya miundo misingi mibovu, ukosefu wa soko, utepetevu wa wafanyakazi na uongozi duni. Kweli si kweli?

Ndwea: Kweli. Tunajaribu jaribu kulitatua hilo.

Mzungu 1: (*Kama ambaye hajasikia lolote.*) Kampuni ya ujenzi wa nyumba **Red Ash** imelegea kwa kiwango kikubwa na hata baadhi ya wafanyakazi wa juu kujiuzulu

huku wakihamia nchi zingine. Sababu ni kwamba baadhi ya wanaopewa nafasi za uhandisi hawana taaluma hizo za uhandisi. Matokeo hasi ya hili ni gorofa mbili zilizoangukiana mwezi jana na kusababisha vifo vya watu zaidi ya miatatu.

Choche: Ni ukweli ila hiyo ilikuwa ajali tu.

Mzungu 1: (*Akipuuza maneno ya Choche*) Kampuni ya kutengeneza magari ilianguka huo huo mwezi jana kwa sababu ya pesa kutoweka bila sababu. Wafanya kazi waliokuwemo wamelalamika kutopokea mishahara yao mpaka leo. Walipojaribu kugoma walifutwa kazi na kiongozi wa nchi ambaye alikuwa msimamizi wa akaunti ya kampuni.

Ndwea: Bwana mkubwa kidogo nipate kueleza pale. Chumvi imetiwa mahali...

Mzungu 2: Utapewa nafasi yako.

Mzungu 1: Chuo Kikuu Cha **NYOTA** kilifungwa kwa sababu ya upotovu wa Naibu chanzela. Wanafunzi waliandamana mara nyingi bila matakwa yao kushughulikiwa. Baadhi ya matakwa ilikuwa kutoratibu mitihani, kuondolewa kwa stima. Kuongezeka kwa karo kila mara na hata ukosefu wa ulinzi. Wengi wa wanafunzi

waliuliwa na majambazi kila mara. Jina la naibu chanzela huyo ni George Choche.

Choche: Hilo ni kweli nilikuwa...

Mzungu 1: Nadhani hatupo kwenye majibizano. Naeleza kinachoendelea katika nchi hii. Hivi juzi nchi hii imezika binti wa miaka ishirini na tatu ambaye alikuwa kiongozi wa wanafunzi katika Chuo Kikuu Cha Sarina. Kifo cha mwanafunzi huyo kilifanyika ndani ya ofisi ya mtemi. Kesi iliposikilizwa mtemi alisema kwamba aliamuru askari wampige risasi baada ya binti yule kumwinulia kisu.

Mzungu 2: Kuongezea, Chuo hiki ambacho ndicho pekee kimesalia na nguvu nchini humu, kimekuwa kikiwapoteza wanafunzi mara kwa mara kwa sababu ya ukosefu wa ulinzi. Utafiti unaonyesha kwamba angalau watu watatu wa jinzia ya kike hufariki chini ya siku thelathini. Bila kuongezea wa kiume ambao utafiti huo unaonyesha hufa angalau mmoja chini ya siku hizi thelathini.

Mzungu 1: Bwana mtemi, haya na mengine mengi yanahitaji maelezo.

Ndwea: Naam, nitaeleza, kwanza kabisa...

Mzungu 2: Usitueleze sisi, utatoa maelezo yako mbele.

Tunatoka sasa hivi.

Ndwea: (*Anatetemeka*) Ta...ta...tafa... Tafadhali naomba msamaha!

Choche: Tuwieni radhi tafadhali! (*Anasimama*)

Mzungu 1: Radhi gani? Wewe mwanzo hicho **Chuo Kikuu cha NYOTA** kirudi hai mara moja

Mzungu 1: Je, wewe ndiwe mtemi wa Sarina?

Ndwea: (*Ameanza kutiririka kijasho tena.*) Ndio. Tafadhali...

Mzungu 1: Una hakika ulistahiki huu uongozi?

Ndwea: Nilipigiwa kura.

Mzungu 2: Nilipigiwa kura! Waafrika mtadanganyana mpaka lini? Damu yenu mwaifyonza wenyewe. Mtakimbilia wapi baadaye?

Mzungu 1: Haya tuondoke. (*Askari mzungu anamsukuma zaidi*)

Mzungu 2: Tembea twende, unatupotezea muda. (*Askari mzungu anamsukuma nje*)

Mzungu 1: Dunia haina mkuu.

Mzungu 2: Wala haina mwenyewe. (*Taa zinazima taratibu*)

GIZA

MWISHO WA MCHEZO

SHEREHE

Shaka Wasiwasi

Sonono Huzuni

Tobokea puani Mambo mabaya mtu aliyotenda kumrudi.

Nyerezi Nzuri

Shani Ajabu

Ukata Umaskini

Kijiti kuonekana mlingoti Jambo ndogo kuonekana kubwa.

Vipeni kuchani Pesa kidogo mtu kukupa.

Tukizi Nadra kufanyika au kutokea.

Kata kiu Jangwani Leta ukombozi.

Juludi Maumbile ya ngozi ya mtu.

Kula mwande Kukosa ulichokitaka.

Lungurisha Fanya mtu kupokea hongo.

Jubilee ya kalenda Miaka ishirini na tano gerezani.

Mori Hasira.

Katisha maini Kuhuzunisha.

Ghawazi Pesa/ hela.

Walitima Watu maskini.

Wakembe Watoto wadogo.

Maasi Mambo maovu.

Fanyia shere Fanyia mzaha.